# Nipashe

Ijumaa Mei 3, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579908

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.fa ipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**JPM AFICHUA NJAMA**

RAIS John Magufuli, amefichua njama anazofanyiwa Mbunge wa Mbarali, Haroub Mohamed (CCM), zikiwamo kuwekewa bunduki...

UKURASA 5



**KIBANO MAJI**

MIRADI ya maji imekuwa kaa la moto kwa Wizara ya Maji baada ya wabunge kuibana vikali wakisema watendaji...

UKURASA 5

UKURASA 13

# HUZUNI



- **Dk. Reginald**

Mengi afariki dunia, Rais Magufuli, UN, mataifa, umma wamlilia... *Endelea ukurasa 2,3&4*

**1942-2019**

**MICHEZO** **WADAU WA MICHEZO WAMLILIA DK. MENGI** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6



HUZUNI 1942 - 2019

# JPM, UN, Marekani wa

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi Dubai, Falme za Kiarabu.

Dk. Mengi ambaye alizaliwa Mei 29, 1942, ni mmoja wa mabilionea barani Afrika, alipatwa na umauti usiku wa kuamkia jana, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na familia yake.

Baada ya taarifa za msiba huo kutolewa na vyombo vya habari vya runinga na redio vya IPP, taasisi za kitaifa na kimataifa na makundi mbalimbali ya kijamii yalionyesha kuguswa na msiba huo na kutuma salamu za rambirambi kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Rais John Magufuli ni miongoni mwa walioguswa na msiba huo ambaye aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter akisema: "Nimesikitishwa na taarifa za kifo cha mzee na rafiki yangu, Dk. Reginald Mengi.

'Nitamkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya taifa letu na maono yake yaliyopo katika kitabu cha 'I Can, I Must, I Will'. Poleni wanafamilia, wafanyakazi wa IPP na Jumuiya ya Wafanyabiashara."

Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas pia aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter akisema: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Dk. Mengi. Kama alivyopata kusema yeye mwenyewe siku za uhai wake kuwa 'watu wanaoacha alama hawafi', basi mawazo, falsafa, ubunifu na kujitoa kwake vitaendelea kuishi nasi."

Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini, Alvaro Rodriguez, pia aliandika katika ukurasa wake wa Twitter akisema: "Ninasikitika sana kusikia kuhusu kifo cha Dk. Mengi. Naungana na Watanzania katika kumlilia ndugu yetu. Fikra zetu na sala zetu zipo pamoja na familia yake. Pumzika kwa amani Dk. Mengi."

Ubalozi wa Marekani nchini pia ulitoa taarifa jana ukieleza kuwa umepokea kwa majonzi taarifa ya kifo cha mfanyabiashara huyo.

"Tulipata fursa ya kufanya kazi na Dk. Mengi katika siku zilizopita na kwa hakika mchango wake katika ukuaji wa muda mrefu wa uchumi na maendeleo ya Tanzania ni mkubwa na muhimu mno.

"Tunatoa pole na rambirambi zetu za dhati kwa familia na rafiki zake na kuungana na watu wa Tanzania katika kuomboleza msiba huu mzito," taarifa ya ubalozi huo

## Wanataaluma waomboleza

**Na Christina Haule,** DODOMA

WANATAALUMA ya Habari wanaoshiriki maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani yanayofanyika jijini Dodoma, wameeleza kupokea kwa mshituko mkubwa kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi.

Akisoma taarifa ya wanataaluma hao jana, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Uhuru Media, Ernest Sungura, alisema Dk. Mengi ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), atakumbukwa daima na wanataaluma ya habari nchini kutokana na kujitolea kwake katika kuimarisha tasnia ya habari nchini.

Alisema Dk. Mengi alianzisha vyombo mbalimbali vya habari, vikiwamo magazeti, redio na runinga Tanzania na Afrika Mashariki.

"Wanataaluma ya habari tunaoshiriki maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, jijini Dodoma, tunatoa pole kwa wanafamilia ya Dk. Mengi, wafanyakazi wa kampuni ya IPP na wanataaluma wote wa tasnia ya habari kutokana na kifo hicho.

"Tunawasihi wanafamilia ya Dk. Mengi na watu wote walioguswa na msiba huu kuwa na ujasiri na uvumilivu ka wakati huu mgumu wa kuondokewa na mpendwa wetu. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe," alisema Sungura.

Baada ya kutolewa taarifa hiyo kabla ya kuanza kwa mkutano wao, wanataaluma wa habari walisimama kwa dakika moja kwa ajili ya kumkumbuka Dk. Mengi.

## ...Bunge lazizim

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA



Anthony Mavunde




Freeman Mbowe



James Mbatia



Livingstone Lusinde



Lucy Owenya



Nape Nnauye

BUNGE jana lilizizima kwa simanzi, baada ya kupokea taarifa za kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk Regnad Mengi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Januari Makamba, alisema kifo chake ni pigo kubwa kwa nchi.

"Nimepokea taarifa hiyo kwa masikitiko na mshtuko mkubwa, kwamba mzee Mengi ukizungumza historia ya biashara, media (vyombo vya habari) hapa nchini, jina lake lazima liwepo na amekuwa pioneer (mwanzilishi) au mtengeneza njia kwenye tasnia ya habari nchini.

"Hapa mwishoni amekuwa ni mtu ambaye ametoa mchango mkubwa kwenye masuala ya jamii, makundi mbalimbali kama walemavu, kwenye haramabee zinazohusu masuala ya jamii alikuwa mstari wa mbele na kuchanga kwa moyo. Amegusa maisha ya watu wengi sana na kwa kweli tutamkosa kama taifa kwa sababu ametoa mchango mkubwa sana karibu katika kila eneo la uhai wa nchi yetu, kwenye uchumi kwenye biashara. Ni pigo kubwa kwa nchi, pigo kwa wanafamilia yake na IPP Media na sisi watu wa serikali na wanasiasa."

**MBATIA**

Mbunge wa Vunjo (NCCR-Mageuzi) James Mbatia, akizungumzia kifo cha Dk. Mengi alisema, "Niombe Watanzania tuwe na utulivu wa ndani hasa wanatasnia ya habari nchini, sekta binafsi nchini na familia yake. Inanibidi nitafakari zaidi na wote tusimtafakari Mengi kama mfanyabiashara, tumuone Mengi akiwa Mtanzania mwenye sura ya uzalendo wa taifa la Tanzania, siyo utajiri wake, bali kama Mtanzania wa kawaida."

Alisema katika uhai wake, Dk. Mengi hakuogopa kupambana kujitoa kwa ajili ya maslahi ya mapana ya Tanzania iweze kuwa sehemu salama na nzuri zaidi ya kuishi.


Mbatia aliwasihi Watanzania, kwa kipindi hiki cha maombelezo, udhaifu wa kibinadamu inabidi uzuiwe na kuwa na utulivu wa ndani, kutafakari, kujiuliza na kuchukua mema yote aliyoifanyia taifa hili badala ya kuzungumza udhaifu wa kibinadamu ambao kila mtu anao.

**MAVUNDE**

Aidha, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya kazi na ajira, Anthony Mavunde, ambaye pia ni Mbunge wa Dodoma Mjini, alisema Mengi ni kati ya Watanzania wachache walioacha alama kubwa katika taifa.

Alisema mwekezaji huyu mzawa, amekuwa ni mtu mwenye msaada kwa watu wengi wenye uhitaji na hasa watu wenye ulemavu ambao watamkumbuka sana kwa mchango wake mkubwa wa kubadilisha fikra, mitizamo lakini pia kuwawezesha kiuchumi kufikia ndoto zao kwamba na wenyewe wanaweza wakasimama na kujitegemea.

"Mzee Mengi anaacha funzo kwa watu wote katika taifa letu, Afrika na duniani, Mwenyenzi Mungu akikujalia mali, uwezo basi hakikisha unashirikiana na wale wenye mahitaji na kubadilisha maisha yao ili iwe sehemu ya sadaka yako. Mengi ametoa sadaka yake kwa kiwango kikubwa sana. Taifa limempoteza mtu mashuhuri, mtu ambaye alikuwa ana upendo mkubwa sana, mtu mzalendo ambaye alikuwa anatamani kuona sekta binafsi inakua na kuzalisha akina Mengi wengi zaidi,"



# amlilia Dk. Mengi

ilieleza.

Rais mstaafu wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Dk. Joseph Kabila, alisema kifo cha Dk. Mengi ni pigo kubwa kwa Tanzania na nchi za Afrika Mashariki na Kati.

"Dk. Mengi ni mtu ambaye alikuwa na ubunifu, aliunda kampuni nyingi zilizoajiri watu wengi Tanzania, alikuwa mfano katika watu wengi kwenye eneo hilo, vijana katika maeneo haya wanaweza kuiga mfano ili kuuendeleza ukanda mzima wa Afrika Mashariki na Kati," Dk. Kabila alisema katika ujumbe wake wa salamu za rambirambi.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akiwa nyumbani kwa Dk. Mengi jijini Dar es Salaam jana, alisema: "Marehemu ni ndugu yangu, tunatoka eneo moja, ni mjomba wangu, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa watu wa Hai, alikuwa mtu wa kipekee kabisa."

Mwenyekiti wa Chama cha Umma (Chaumma), Hashim Rungwe, katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema chama chake kimepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Dk. Mengi kwa kuwa alikuwa na mchango mkubwa kwa taifa.

Rungwe alisema Dk. Mengi ameisaidia nchi kiuchumi, kiafya, kimichezo, hivyo kifo chake ni msiba wa taifa kwa kuwa katika maisha yake, alimgusa karibu kila mtu.

Kiongozi mstaafu wa Vijana Barani Afrika, Francine Muyumbai, alisema Dk. Mengi ameacha pengo kubwa kwa kuwa alikuwa akiwapa vijana wengi wa Afrika kazi kupitia kampuni zake.

Waziri wa zamani wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Nape Nnauye, alisema: "Umeacha alama kubwa, nimejifunza mengi kwako, rafiki, mshikaji, kiongozi na mzazi, ulinifundisha kuwa kukata tamaa ni

INAENDELEA UK.8


# a kwa simanzi



January Makamba



Joseph Mbilinyi



Juma Nkamia



Pendo Peneza



Peter Msigwa



Selemani Zedi

**PENEZA**

Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Upendo Peneza, amemlilia Dk. Regnald Mengi akisema, "Kwangu mimi mzee Mengi nimemfahamu miaka mitano iliyopita, nikiwa nagombea nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Taifa la Chadema (Bavicha), yeye aliniona kwenye kipindi cha asubuhi kwenye TV moja, baada ya kuniona akaenda akaandika kwenye twitter kwamba 'nina muangalia binti Upendo Peneza, ni binti ambaye ana uwezo na uelewa mpana na kwangu mimi Upendo ni shujaa.'

"Ile twitt ambayo aliandika, kiukweli ilinisaidia kwa namna fulani kwenye kipindi cha kampeni ile kwa maana alitambua uwezo wangu, nikawa naitumia kuomba kura kwenye nafasi hiyo kwenye ngazi ya kitaifa na pia baada ya ku-twitt alitafuta namba yangu mwenyewe akanipigia simu tukaongea, akanitia moyo na akaniambia niendelee na jitihada hizo za kutafuta nafasi katika uongozi mpaka hatimaye nikawa Mbunge. Kwangu mimi ndiye aliyeshika na kufungua safari yangu ya kisiasa."

**LUSINDE**

Pia, Mbunge wa Mtera (CCM), Livingstone Lusinde, alisema Mengi ni alama ya matajiri wachache wenye unyenyekevu kwa Mungu, lakini matajiri wachache wenye utu, ameacha alama kubwa ya kusaidia watu maskini, watu wenye ulemavu na watu wenye mahitaji mbalimbali.

Alisema katika maisha yake amekuwa kioo na mfano mkubwa sana wa kujinyenyekeza mbele za wenzake.

**NKAMIA**

Mbunge wa Chemba (CCM), Juma Nkamia, amemuelezea Reginald Mengi kuwa ni mmoja kati ya watu waliofanya transiformation (mabadiliko) ya habari Tanzania.

"Hakika huu ni msiba mzito, misiba yote ni mizito, lakini misiba inatofautiana, Watanzania tumepoteza mtu muhimu sana," alisema Nkamia.

Mbunge wa Sumve (CCM), Richard Ndasa, ameeleza kuwa msiba huo ni mzito kwa taifa, pengo aliloliacha ni kubwa kwa sababu ni mmoja wa wawekezaji wakubwa katika nchi yetu kwa hiyo kila mtu anafahamu mchango wake katika uchumi wa nchi yetu, ajira ambazo alikuwa anazitoa, lakini uwekezaji wake.

**MSIGWA**

Mbunge wa Iringa Mjini Chadema), Mch. Peter Msigwa, amemuelezea Dk. Mengi kuwa amewahamasisha kwa kiasi kubwa taifa kufikia ndoto za kiuchumi na amekuwa mshiriki na mdau mkubwa wa maendeleo.

"Najua mzee Mengi alikuwa mwanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM), lakini alikuwa na siasa za kistaarabu na aliheshimu watu wote ambao hawakuwa wanachama wa chama tawala," alisema Msigwa.

**ZEDI**

Naye, Mbunge wa Bukene CCM), Seleman Zedi, alisema tangu amfahamu Mengi kama mtu ambaye amefanikiwa kiuchumi, lakini wakati wote

INAENDELEA UK.8

# THRDC: Mengi alikuwa muhimu sekta ya habari

Na Salome Kitomari

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umesema utamkumbuka Dk. Regnald Mengi, kwa jitihada kubwa za kuboresha upatikanaji wa habari na sekta ya habari nchini.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema tangu mwanzoni mwa miaka ya tisini hadi kifo chake, Dk. Mengi alikuwa mstari wa mbele katika kuwekeza kwenye sekta ya habari katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Hii inathibitika kwa kuangalia jitihada alizozichukua kwa kuanzisha vituo vya redio kama Radio One na Capital Radio; vituo vya television kama ITV, EATV na Capital TV; pamoja na magazeti yakiwamo The Guardian na Nipashe," alisema.


Alisema vyombo hivyo vya habari vimefanya kazi kwa mafanikio makubwa, huku vikifanikiwa kuwa mfano wa kuigwa na vyombo vingine vya habari nchini.

Alisema Mengi atakumbukwa sana kutokana na mchango wake katika kupigania uhuru wa kujieleza na haki ya kupata taarifa.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo, kwa zaidi ya miaka saba, TRDC umekuwa ukipata ushirikiano mzuri kutoka kwa Mengi hasa katika kutetea na kuimarisha ulinzi na usalama wa wanahabari nchini.

Alitolea mfano Mei 15,mwaka 2013, wakati Mengi alipokuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), Mtandao ulipata ushirikiano mkubwa kutoka kwake katika kufanya mkutano wa mashauriano na kuboresha umoja kati ya watetezi wa haki za binadamu na wamiliki wa vyombo vya habari ili kuboresha ulinzi na usalama wa waandishi wa habari nchini.

"Kufuatia kifo cha mtu huyu muhimu kwenye historia ya vyombo vya habari, wakati huu ambao wadau wa habari wanasubiri kusherehekea Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani kesho (leo), Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania unatoa pole kwa familia,wana IPP na marafiki wote," alisema.



HUZUNI 1942 - 2019

# DK. MENGI ALIVYOTUMIKIA JAMII YAKE

Na Romana Mallya

NI wastani wa wiki nne kasoro siku moja, kutimia tarehe ya kuzaliwa kwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia juzi.

Ni pigo kubwa katika jamii, pande zote za imani na umma, kutokana na umuhimu wake katika jamii.

Ni mzaliwa wa Mei 29, mwaka 1942, katika kijiji cha Nkuu, kilichopo Machame mkoani Kilimanjaro. Katika kipindi chote cha maisha anayojitambua, aliamini katika falsafa, "kufa maskini ni mtu kujitakia."

Kupitia falsafa hiyo, imemvusha kutoka nyumba ya umasikini na kuingia katika historia kuwa miongoni mwa waliofanikiwa kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania na barani Afrika kwa jumla.

Alikuwa na kawaida kimaisha. Mara nyingi kila alipokutana na makundi mbalimbali kwenye jamii, bila ya kujali ama yamefanikiwa au la, aliwataka watu hao wakatae umaskini, akirejea kwamba ndivyo ilivyokuwa tabia yake.

Alirejea kwamba, ndivyo alivyokuwa katika zama za ujana wake, alihangaika mno kujikwamua kutoka mahali alikosimama, kuelekea katika kundi la waliofanikiwa au matajiri wa nchi.

Miongoni mwa vitu ambavyo Dk. Mengi atakumbukwa nayo ni namna alivyoshiriki kitaifa kuhakikisha makundi mbalimbali kwenye jamii yanapambana na umaskini na kujikwamua kimaendeleo, ili kuisaidia nchi kufikia uchumi wa kati wa viwanda.

Zama za uhai wake zilizoishia usiku wa kuamkia jana, alidumu kushiriki katika mambo mbalimbali ya kijamii, hususan kusaidia makundi tofauti ya kijamii walio wahitaji.

Hapo inawajumuisha walemavu, yatima, wajane na wengine wanaojiweza, kwa kutoa ushauri na misaada ya namna ya kulinda nafasi zao kwenye jamii.

Katika kuhakikisha kundi kubwa la vijana wa sasa na taifa lijalo linabaki na kumbukumbu ya maisha yake kwa dhana ya kuuchukia umaskini na kujikomboa, Dk. Mengi aliaandika kitabu kilichosheheni historia pana ya maisha yake ya umaskini alioupitia hadi kufikia mafanikio yake.

'I Can, I Must, I Will' ndicho kitabu cha Dk. Mengi ambacho makundi mbalimbali kwenye jamii, kila siku yanaendelea kukinunua, kufahamu na kujifunza mbinu alizotumia wakati huo akiwa katika zama za umaskini wake, hadi kufikia mafanikio aliyonayo.

Julai 2, 2018, Dk. Mengi alizindua rasmi kitabu hicho mbele ya Rais Dk. John Magufuli, ambacho sasa licha ya kwamba kimwili hayupo, kupitia kitabu hicho Watanzania wataendelea kumuenzi, kuishi na kujifunza namna ya kujikwamua na umaskini.

Akisimulia historia ya maisha yake mbele ya Rais Magufuli na wageni wengine kutoka ndani na nje ya nchi waliohudhuria sherehe za uzinduzi wa kitabu hicho siku hiyo, Dk. Mengi alisema alizaliwa katika familia maskini, lakini maishani mwake hakuwahi kuukubali umaskini.

"Leo nitawaeleza nilikotoka, nilipo na ninakokwenda, kwanza sioni aibu kusema nilizaliwa kwenye umaskini uliopindukia," alianza kusimulia na kuongeza:

"Nilizaliwa kwenye nyumba udogo ya msonge ikichanganywa na ng'ombe, mbuzi panya hata mende.

"Leo nimesimama mbele yenu kama mpambanaji wa kupambana na umaskini. Kilichonitoa huko kwenye umaskini, ni kwa sababu sikuuona kama ni tatizo, bali changamoto.

"Unapotembea kila mahali ukasema 'umaskini, umaskini, umaskini' utazidi kuwa maskini unapaswa kusema umaskini utaachana nao, kwa sababu ni changamoto tu."

Dk. Mengi alisema, baada ya kuona umaskini ni changamoto, ni lazima mtu awe na macho yanayoona fursa, akiamini ndicho kilichomfikisha alipo.



Dk. Reginald Mengi, akisalimiana na Rais mstaafu wa Nigeria, Jenerali Olusegun Obasanjo, walipokutana katika Mkutano wa Eneo la Biashara Huru Barani Afrika, ulioandaliwa na Umoja wa Afrika (AU), mjini Kigali, nchini Rwanda Machi 21 mwaka jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**CHIMBUKO LA KITABU**

Kuhusu kitabu chake, Dk. Mengi alisimulia uamuzi wa kukiandika kutokana na makundi ndani ya jamii, alipokutana nayo yalimuuliza kwa nini kitabu hicho, 'I Can, I Must, I Will'.

"Nilikuwa na mtoto anaitwa Rodney (Motie), ambaye kabla Mwenyezi Mungu hajampokea, kabla hajaondoka duniani aliniomba sana niandike kitabu, alisema na kuendelea:

"Aliwahi kuniambia baba nataka uandike kitabu kitakachoelezea maisha yako na mambo uliyofanya ambayo ninayafurahia sana. Naamini wengine watayafurahia wakisoma, nilimwambia nitafanya hivyo."

Dk. Mengi alisimulia kuwa kitu kilichomsukuma kuandika kitabu, ni kwa sababu ya kupitia maisha ya umaskini na kuamua kuyakataa, akisema anaweza.

"Niliamua kuandika kitabu cha kuelekezea namna nilivyoachana na umaskini, kwa sababu siyo watu wote wanatoka katika familia bora. Wengi ni maskini, ila wakisema wanaweza, wanaweza kweli," alisema.

Akiwaelezea wazazi wake, Dk. Mengi alisimulia kwamba mama yake alikuwa akienda soko la Kalali (Moshi) kununua ulezi na aliporudi nyumbani aliuweka maji kabla ya kwenda kuuuza ili uwe mzito.

"Alikuwa akiuweka maji ili uwe mzito kisha anaupeleka soko lingine kuuza. Wakati huo alikuwa anauza kwa kilo, kwa hiyo ulikuwa na uzito mara mbili au tatu," alisema.

Pia, alisema baba yake alikuwa ananunua kondoo, kisha anawasafisha na siku ya kuwauza, alikuwa akiwapa maji na kuwauza bei kubwa zaidi, kutokana na kuongezeka uzito.

**DARASA LA KAKA**

Kuhusu kaka yake, alisema aliomba wazazi fedha kidogo ya mtaji akapewa na alianza kuuza mayai matano na baadaye biashara ilikuwa hadi kuwauzia polisi.

"Siku moja usiku alifukuzwa na simba mayai yake yote yakapasuka, lakini hakukata tamaa. Alichukua trei nyingine ya mayai na kuendelea.

"Wakati akifanya biashara hiyo, aligundua kuwa polisi wanavaa viatu vinavyong'aa, hivyo akaomba awe anawang'arishia viatu ili mwisho wa mwezi wamlipe.

"Walikubali na alipopata fedha za kutosha, alirudi nyumbani akanunua gari aina ya pick up (gari dogo la kubeba mizigo), akawa anabeba bidhaa kwenda Mombasa kwa uaminifu. Kuna kitu alinifundisha, uaminifu katika biashara," alisema.

Dk. Mengi alisema jambo kubwa ambalo mama yake mzazi alimfundisha, ni kutoa kwa watu wenye njaa kali. Alieleza:

"Ninakumbuka siku moja mama yangu alipika chakula akawapa watoto waliokuwa na njaa, sisi akatuambia tusubiri kwanza. Huu ndio upendo ambao mama alitufundisha kuwajali wengine".

**MASOMO YAKE**

Dk. Mengi alianza elimu ya msingi, katika Shule ya Msingi Kisereny Village Bush, kisha akajiunga na Shule ya Nkuu District, baadaye Shule ya Siha, zote za mkoani Kilimanjaro.

Baada ya elimu ya msingi, sekondari alipata katika Shule ya Old Moshi. Mara baada ya kuhitimu shule, Dk.Mengi alipata ufadhili wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahawa Mkoa wa Kilimanjaro (KNCU) alipoenda nchini Uingereza kuchukua masomo ya Uhasibu na kurudi Tanzania mwaka 1971.

Baada ya kurejea nchini, aliajiriwa kwenye kampuni ya Coopers and Lybrand Tanzania, ambayo kwa sasa inajulikana kama Price Waterhouse Cooper.

Baada ya kufanya kazi kwa muda mrefu, alijiengua na kuanzisha kampuni katika miaka ya 1980, ambayo ikaunda Kampuni za IPP (IPP Group of Companies).

Kampuni hiyo anzilishi ilijishughulisha na kutengeneza kalamu za wino na baadaye ilipanuka na kuwa wazalishaji wakubwa.

IPP Group of Companies, ndio ilimuwezesha Dk. Mengi kuanzisha vyombo vya habari akianza na ITV/Radio One, kisha kufuatiwa na redio na televisheni za EATV na Capital.

Aidha, hatua hiyo pia iligusa uanzishaji magazeti baadhi yake ni; The Guardian, Nipashe, Sunday Observer, Kulikoni, Taifa Letu, Financial Times, Alasiri na Lete Raha, zote chini ya kivuli cha umiliki wa kampuni ya magazeti,The Guardian Limited.

Kampuni ya IPP Group ya Dk. Mengi, mbali na vyombo vya habari, inajumuisha viwanda vinavyozalisha vinywaji baridi, wazalishaji wa maji ya Kilimanjaro, pia soda zinazozalishwa na kampuni ya Bonite Bottlers, wazalishaji wa soda aina tofauti, chini ya kivuli cha Coca-Cola.

"Dk. Mengi pia alikuwa na utashi katika sekta ya madini, mafuta na gesi," inatamka taarifa ya familia.

Pia, taarifa inataja maeneo mengine ambayo ni mwelekeo wake mpya wa kibiashara ni katika uundaji magari, kiwanda cha dawa, na uzalishaji saruji.

**NAFASI ZA UONGOZI**

Katika eneo la uongozi ana historia ndefu, ikiwamo katika nafasi za uongozi wa umma.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi ya kifamilia, Dk. Mengi alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni ya Tanzania Standard Newspapers, wachapishaji wa magazeti ya Daily News na Habari Leo.

Aidha, ameshakuwa Kamishna wa Kamati inayoshughulikia mishahara na Mwenyekiti wa Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA), pia Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mazingira Tanzania (NEMC).

Nyingine ni, Mwenyekiti wa Vyombo vya Habari vya Jumuiya ya Madola Tanzania (CPU), Mkurugenzi wa Bodi ya asasi ya Leadership for Environment and Development International (Lead); Kamishna wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids); na Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI).

Nafasi nyingine ni, Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC ); Mwenyekiti wa Kamati ya Mabaraza ya Kimataifa ya Biashara (ICC); na Mkurugenzi wa Bodi ya Baraza la Biashara la Jumuiya ya Madola (CBC).

Pia, ameshakuwa, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) aliyostaafu mwaka jana alimkabidhi mwenziwe.

Amekuwa Mlezi wa taasisi ya Jane Goodall Tanzania; na mmoja wa wadhamini wa Kituo cha Mafunzo ya Kichina (CCS) kilichopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nafasi hizo mbili alikuwa anaendelea navyo.

Katika tasnia ya habari, hadi umauti unamfika ni Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT).

**TUZO ZAKE**

Katika zama za uhai wake amepata tuzo nyingi zisizopungua 38, zikijumuisha vyeti na utambuzi rasmi, vyote vikitoa ujumbe mazuri aliyotenda katika jamii.

Baadhi ya nafasi hizo kwa mujibu wa taarifa hiyo ya familia ni kama ifuatavyo:

* Mwaka 1994, Dk. Mengi alipewa tuzo ya 'The Order of the United Republic of Tanzania' mwaka 1995 'The Order of the Arusha Declaration of the First Class'

* Mwaka 2008 alipata tuzo nchini Marekani ya 'The Martin Luther King Jr Drum Major for Justice' na mwaka 2014 Jumuiya ya Kimataifa ya Lions Club ilimpa tuzo ya 'The International Order of the Lions Club'

*Mwaka 2012 Taasisi ya Oslo ya Sweden ijulikanayo kama Business Peace Foundation ilimpa tuzo ya 'The 2012 Business for Peace Award' baada ya kupendekezwa na kamati inayotoa tuzo za Nobell.

* Mwaka 2014 katika sherehe za miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Rais mstaafu Jakaya Kikwete alimpa tuzo ya taifa katika mambo ya kusaidia na kuiwezesha jamii hasa katika ujasiriamali wa kijamii 'The National Philanthropy Award'

## HABARI KITAIFA



Rais Dk. John Magufuli, akizungumza na wananchi baada ya kuzindua Hospitali ya UWATA, jijini Mbeya jana. **PICHA: IKULU**

# JPM afichua bunduki kufichwa kwa mbunge

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli, amefichua njama anazofanyiwa Mbunge wa Mbarali, Haroub Mohamed (CCM), zikiwamo kuwekewa bunduki kwenye shamba lake kwa lengo la kumchafua.

Vilevile, amesema mbunge huyo ameundiwa kundi la watu ambao wanalipwa pesa na watu wenye nia ovu dhidi yake.

Rais Magufuli alifichua njama hizo jana katika mkutano wa hadhara alioufanya katika Viwanja vya Rujewa wilayani Mbarali ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake mkoani Mbeya.

"Changamoto nyingine iliyopo Mbarali ni majungu, mtaicheleweshaa kwenda mbele, ninajua wapo watu ambao wamelipwa hela, wamepangwa kuja kumzomea mbunge, haya hayatawasaidia, ukiwa unataka ubunge, usububiri wakati, subiri uje umshinde kwenye kula, lakini haya majungu yanawachelewesha," alisema.

Rais Magufuli aliongeza: "Majungu hayajengi, ninawaambia ndugu zangu kwa dhati kabisa, mnapochagua watu hamchagui malaika, huyu ni mbunge wa kuwatumikia watu, mmepanga kumchafua, hatachafuka.

"Mmefanya mengi ya ajabu, mkaenda kwenye shamba lake mkaenda kufukia silaha ambazo wala siyo zake kwa umiliki, msifikiri hatujui, acheni mambo ya namna hiyo na bahati nzuri wanaofanya hayo wanajulikana, kama hizo ndizo mbinu za kupata ubunge hupati, mimi ndiyo mwenyekiti."

Rais Magufuli pia aliaziga apewe majina ya watu waliopewa hekta 5,900 ambazo serikali iliagiza zirudishwe kwa wananchi kutoka kwa wawekezaji.

"Ninachotaka hizo hekta nipate orodha ya watu waliopewa, mnipangie orodha, kwamba huyu ni fulani amepewa hekta kadhaa, ili hekta hizi 5,900 zijulikane wamepewa kina nani, inawezekana zikawa hewa.

"Haiwezekani wananchi wote wa Mbarali mimi nimetoa ardhi halafu wao walalamike kwamba hawajapata ardhi wakati mimi

INAENDELEA UK. 8

# Miradi ya maji kaa la moto kwa Mbarawa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MIRADI ya maji yakiwamo mabwawa ya umwagiliaji yamegeuka kaa la moto kwa watendaji wa Wizara ya Maji, baada ya Wabunge kudai mingi inayotekelezwa sasa fedha zake zimeibwa na makandarasi.

Wamesema wanashirikiana na baadhi ya watendaji kuichakachua, hivyo kukwamisha juhudi za serikali.

Akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/20, Mbunge wa Nkasi (CCM), Ally Kessy, alimtaka Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa kuunda tume kuchunguza wizi huo, akidai kuna baadhi ya watumishi wa wizara wanahusika kwenye ubadhirifu wa miradi ya maji wakishirikiana na baadhi ya makandarasi.

Kessy aliahidi kumtaja kwa jina na kumshtaki kwa Rais John Magufuli, Waziri aliyedai kumtishia (hakumtaja jina) baada ya kumueleza ufisadi unaofanyika katika jimbo lake.

"Makandarasi wamezidi, kwa nchi nzima kumekuwa na uchakachuaji wa hali ya juu ya miradi ya maji na ndio imekuwa ikitumika kuiba fedha za miradi. Makandarasi wanashirikiana na maofisa kuiba fedha za miradi ya maji, Mheshimiwa Waziri unda tume, kagua mradi kwa mradi nchini nzima, wilaya kwa wilaya na mkoa kwa mkoa ili wale waliofanya ubadhirifu wa fedha watapike fedha mara moja, hakuna huruma.

Aliongeza: "Kuna waliojenga maghorofa na majumba kwa ajili ya miradi ya maji ya nchi hii, mimi ushahidi ninao maana yake

INAENDELEA UK. 8


**TANZANIA INVESTMENT CENTER (TIC)**

**TANZANIA - CHINA BUSINESS FORUM**

**ARUSHA INTERNATIONAL CONFERENCE CENTRE (AICC) – 13TH MAY 2019**

**Tanzania Investment Center (TIC)** in collaboration with the Tanzania Private Sector Foundation (TPSF) and Tanzania Tourism Board (TTB), is preparing a Business and Investment Forum between Tanzanian entrepreneurs and their counterparts from China, who expect to visit the country for tourism and to explore business and investment opportunities.

The forum is scheduled to take place on 13th May, 2019 at the Arusha International Conference Center (AICC) in Arusha at 8:00am.

The targeted sectors are ***mining and Tourism.***

Interested participants are required to confirm their participation not later than 10th May, 2019. For further details and registration, please contact Ms. Diana Ladislaus Cell. No. 0719653079 email: **diana.ladislaus@tic.go.tz** or Mr. Juventus Baitu Cell. No. 0621153276 email: **juventus.baitu@tic.go.tz**

Issued by:

**The Executive Director,**
**Tanzania Investment Centre (TIC)**
**Shaaban Robert Street,**
**PO Box 938, Dar Es Salaam**
**Tanzania**
**Tel +25522116328**
**Website: www.tic.go.tz**

215209102



**LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE**

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA NANE WA WANACHAMA WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**

Kwa wanachama wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu,

Tafadhali fahamu kuwa Mkutano Mkuu wa mwaka wa 18 wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu unatarajiwa kufanyika siku ya Jumamosi **tarehe 25 Mei 2019**. Mkutano huo utatanguliwa na Warsha itakayoanza **Saa 2.30 asubuhi** katika ukumbi wa mikutano wa Justice Lugakingira katika ofisi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu zilizopo Kijitonyama Dar-es-Salaam.

Katika Mkutano huo Ajenda zifuatazo zitajadiliwa:

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Akidi
3. Kupokea Ajenda
4. Kumchagua Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu
5. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa kumi na saba
6. Yatokanayo na kumbukumbu za mkutano wa kumi na saba
7. Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.
8. Taarifa ya ukaguzi wa hesabu za mwaka 2018
9. Kumteua Mkaguzi wa hesabu za Mwaka 2019
10. Kuthibitisha Wanachama Wapya wa Kituo
11. Tarehe ya Mkutano mkuu ujao
12. Mengineyo
13. Kufunga Mkutano

**Tafadhali thibitisha ushiriki wako.**

**Wasalaam,**
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu**

**Bi Anna Henga**
**Mkurugezi Mtendaji**

215210102

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dk. Mengi ametuachia mazuri mengi, yaenziwe

**MWENYEKITI** Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi Dubai, Falme za Kiarabu.

Dk. Mengi ambaye alizaliwa Mei 29, 1942, ni mmoja wa mabilionea barani Afrika, alipatwa na umauti usiku wa kuamkia jana, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na familia yake na kutolewa na vyombo vya habari vya runinga na redio vya IPP.

Taasisi za kitaifa na kimataifa na makundi mbalimbali ya kijamii yalionyesha kuguswa na msiba huo na kutuma salamu za rambirambi kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Ni dhahiri kuwa jamii imeguswa sana na msiba huo mzito na pengine ndio maana wengi wameelezea kusikitika, akiwamo Rais John Magufuli ambaye alisema alieleza kusikitishwa na kwamba atamkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya taifa na maono yake yaliyopo katika kitabu cha 'I Can, I Must, I Will'.

Hatutaweza kueleza kwa undani kila mmoja amesema nini, lakini itoshe tu kueleza kuwa Dk. Mengi alikubalika sana katika jamii kutokana na kujitoa kwake kusaidia watu wengi waliohitaji msaada pamoja na ushauri wa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha.

Katika baadhi ya mambo ambayo mchango wake hautasahaulika ni kujitoa kwake kusaidia watu wenye ulemavu. Kwa takribani zaidi ya miaka 20 amekuwa akiwasaidia watu hao kwa njia mbalimbali ikiwamo kukaa na kula nao chakula kila mwaka, akieleza kuwa anafanya hivyo kwa kuwatambua wa kundi hilo kuwa ni sawa na binadamu wengine.

Kutokana na kuguswa na kuthamini mchango wake huo, serikali ilimshauri kuanzisha taasisi ya watu wenye ulemavu ili na serikali iangalie uwezekano wa kupitisha msaada wa kulisaidia kundi hilo.

Ushauri huo aliuzingatia kwa kuanzisha taasisi hiyo, ambayo aliitumia mwaka jana kutoa tuzo kwa watu wenye ulemavu waliofanya vizuri katika mambo mbalimbali katika jamii.

Pia Dk. Mengi atakumbukwa na jumuiya ya wafanyabiashara ndani na nje, kutokana na mchango wake alioutoa ikiwamo kuongoza taasisi mbalimbali za wafanyabiashara. Miongoni mwa hizo ni Baraza la Taifa ka Biashara (TNBC), Chama cha Wafanyabiashara wa Viwanda (CTI), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chama cha Wafanyabiashara Afrika Mashariki na mkurugenzi katika jumuiya ya wafanyabiashara wa Jumuiya ya Madola, kwa kutaja baadhi.

Kadhalika, Dk. Mengi katika uhai wake alisimamia na kusaidia miradi kadhaa ikiwamo ya kulinda na kuhifadhi mazingira pamoja na ya kupambana na umaskini, ikiwamo kuanzisha vikundi vya kusaidia vijana kupambana na umaskini.

Vile vile, atakumbukwa na wanataaluma wa tasnia ya habari kutokana na uwekezaji mkubwa, ambao uliwezesha wengi kupata ajira pamoja na kutetea haki za waandishi wa habari. Pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT).

Dk. Mengi ameacha alama katika jamii, tukimaanisha kuwa ameacha mazuri mengi ambayo tunapaswa kuyaendeleza kwa lengo la kujiletea maendeleo.


Kitabu chake cha 'I Can, I Must, I Will' ni urithi kwa wengi ambao wana kiu ya kuondokana na umaskini na kupata mafanikio katika maisha, hivyo ni muhimu Watanzania tukakisoma na kuzingatia aliyoyaeleza kuhusiana na siri ya kufanikiwa. Hakika alikuwa mtu wa kuthubutu. Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi. **Amen.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Beatrice Moses

# Vigodoro hadharani vidhibitiwe, vinachochea maadili machafu

**UTANDAWAZI** unaifanya teknolojia ya habari na mawasiliano kuzidi kushika kasi katika sura ya kijiji kimoja. Matumizi ya mitandano ya jamii kupitia 'simu janja' za mkononi (Smart Phone) yametawala kila eneo.

Yapo mambo kadhaa yanayoibuliwa kwenye mitandao, yanayosababisha ama matokeo chanya au hasi kwenye jamii, hasa kupitia baadhi ya video.

Katika mtazamo hasi ambayo si bora kwa jamii, nitazungumzia ngoma ya Vigodoro, ambazo zinaonyesha wanawake wamevaa 'madela.'

Uchezaji wa ngoma hizo inayotawaliwa na mbwembwe za kukosa staha hata kidogo, wanajitikisa katika namna inayotia aibu, wakiwamo watoto.

Binafsi, jambo hilo limenishangaza, japo siyo mara yangu ya kwanza kuona. Ninachoona ni kwanba, hali hiyo inazidi kushika kasi, hivyo inaoyesha kuwa mmomonyoko wa maadili unachukua nafasi zaidi.

Ama itajwe ni ngoma au muziki wa vidogoro, uhali unachukuaku nafasi yake. Wanawake wasiokuwa na 'soni' unaonyesha ujuzi wao wa kutingisha miili katika namna isiyo na chembe ya heshima hata kodogo, wanafaya hivyo pasipo kujali ni wadau wa rika ipi wananagaalia au kuwafuatilia.

Binafsi, najiuliza hili la kimamama wenzangu, kwanini mambo haya hayajadhibitiwi kuanzia kwenye ngazi za vijiji na mitaa, ili kulinda kizazi chetu?

Ni mambo yaliyoambukiza. Siyo ajabu kupishana na wasichana wamevaa 'madela' lakini ikifuatiliwa uhalisia, hakuna staha ya mavazi hata kidogo

Mwenyekiti wa serikali ya mtaa, ndiye mkuu wa serikali ya mtaa husika. Kuna baadhi ya mitaa, inabaki kama vile haina mkuu kutokana na yanayotokea mitaani kwao.

Kuna mitaa ambayo imekithiri kwa vijiwe vya vijana wasio na nidhamu. Baadhi yao wanathubutu hata kuvuta bangi hadharani, yaani wanaonyesha jinsi eneo husika lisivyo na mtawala zaidi yao.

Miongoni mwa nnayoweza kujiuliza, yanatokeaje kwenye mtaa au kijiji ambacho kina uongozi? Kuna sherehe zingine za wanaume ambao nao wana yao machafu zaidi, hayafai kuzungumzwa katika mazingira rasilimali hizo. Niseme tu kuna kashfa, pia fedheha kubwa.

Kutokana na utaratibu wa sheria za mazingira zilivyo sasa, ni vigumu kuandaa sherehe yenye muziki bila ya kuwa na kibali kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa.

Hiyo maana yake ni kwamba, shughuli hizo za kusasambua zinapata vibali kutoka kwa wenyeviti wa mitaa husika.

Pia, viongozi wa dini nao wana mchango mkubwa katika kukabili hilo, wakihakikisha wanashiriki kudhibiti mmomonyoko wa maadili, kwa kusimamia miongozo ya dini zao.

Hapo wanawaonya waumini wao kuwa mbali na ukiukwaji kanuni za kiumini kwa dini tofauti.

Kuna baadhi ya sherehe, ambazo kwenye maeneo kadhaa hasa ya jiji la Dar es Salaam, zimekuwa zikihusisha ngoma kama za 'vigodoro' badala ya kuegemea yale yenye shukrani za kumsifu Mungu.

Imasikitisha, waumini wa imani mbalimbali kujaribu kulishirikisha hilo kwa kualika ngoma za aina hiyo, mitaa ikifunga kwa kelele za shangwe zinazoambatana na lugha zisizo na staha.

Baraza la Sanaa la Taifa (Basata), mwaka 2014 lilikataza Kamati ya 'Miss Tanzania' kutohusisha burudani zinazokiuka maadili ikiwamo ngoma zilizobeba aibu kama vile zilizo maarufu kwa majina; khanga moja, ndembendembe' na 'tisheti ndembendembe ya vigodoro.


Pia mwaka 2016, wizara inayohusika na Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ilitangaza kuufungia wimbo wa Snura au 'Chura' kuchezwa kwenye vyombo vya habari, pia msanii aliyeimba wimbo huo wa Snura, inaufanyia marekebisho.

Kutodhibiti mambo hayo ni hatari kubwa, kwa kuwa inawezekana kuwa kichocheo cha vitendo vya ulawiti na unajisi kwa watoto.

Pia, ni kipingamizi cha udhibiti wa maambukizi mapya ya ukimwi, ikipoteza haki za ukuaji watoto ndani ya maadili.

Vyombo husika vinaaswa kutosubiri malalamiko kutoka kwa jamii, ndio vichukue hatua kudhibiti yote yanayokwenda kinyume na maadili, bali vinapaswa kuhakikisha wanajitanua, kwa kujiongezea wadau zaidi wa kuwapa taarifa za vinavyoendelea kwenye maeneo tofauti ili waweze kudhibiti.

## TANGAZO




# SALAMU ZA RAMBIRAMBI
# KUFUATIA KIFO CHA DKT. REGINALD MENGI

Tumehuzunishwa na taarifa za kifo cha Dkt. Reginald Mengi. Tunatoa pole na rambirambi zetu za dhati kwa familia, marafiki na watanzania kwa ujumla.

Dkt. Mengi alionyesha njia katika ujasiriamali, ujasiri na ukarimu katika shughuli zake nyingi za biashara na kujitolea. Atabaki kuwa kielelezo cha hamasa na matumaini kwa watu wengi Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Alikuwa mshauri mwenye thamani na rafiki kwa sisi wote katika familia ya Coca-Cola na tutamkumbuka katika mioyo yetu milele.

**Pumzika kwa Amani.**

Coca-Cola Kwanza | NYANZA BOTTLING | Coca-Cola BONITE BOTTLERS Co. LTD.

# JPM, UN, Marekani wamlilia Dk. Mengi

INATOKA UK. 3

dhambi, msalimie Mzee Sitta, mkumbushe kile kikao chetu cha mwisho nyumbani kwako, pumzika kwa amani Dk. Mengi."

Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alisema amepokea kwa mshtuko mkubwa kifo cha Dk. Mengi na kwamba kuondoka kwake ni pigo kubwa kwa tasnia ya habari nchini.

"Dk. Mengi amesaidia watu wengi katika kupata ajira kwenye tasnia hii ya habari na wengi wamenufaika kwa kujiendeleza kielimu. "Hata watu wenye vipato vya chini wamenufaika naye, kila mwaka amekuwa akifanya dhifa kwa watu wenye ulemavu ili na nao wajisikie wapo sawa na watu wengine katika jamii, ni pigo kubwa, Mungu amweke mahali pema peponi," alisema.

Mfanyabiashara maarufu nchini Mohammed Dewji 'Mo', aliandika katika ukurasa wake wa Twitter akisema: "Inna lillahi wa inna ilayhi raji'un. Mwenyezi Mungu ampe Dk. Mengi pumziko na ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi."

Lazaro Nyalandu, mbunge wa zamani wa Singida Mashariki alisema: "Poleni sana wana familia, ndugu jamaa na marafiki wa Reginald Mengi kufuatia kuondokewa na mpendwa wetu, Reginald Mengi. Hakika siku za maisha yetu zimehesabiwa na kuandikwa kitabuni. Ameimaliza safari yake hapa duniani. Iwe heri kwake huko ng'ambo ya mto. R.I.P baba yetu."

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, aliandika katika ukurasa wake wa Facebook akieleza kuwa wiki mbili zilizopita walisali na kuongea mambo mengi na Dk. Mengi.

"Nakumbuka nilikutania hebu jaribu kukimbia na ulikimbia kidogo, nilifurahi kuona afya yako inaimarika. Nawaombea wote uliowaacha duniani moyo wa subira, 'R.I.P' (pumzika kwa amani) Reggy," Kasesela alisema.

Kamishna Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania, Grace Kado, ametoa pole kwa familia, wafanyakazi wa IPP, marafiki na tasnia ya habari kufuatia msiba huo.

# Miradi ya maji kaa la moto kwa Mbarawa

INATOKA UK. 5

walitaka kunihonga na mimi nikakataa. Walikuja mpaka bungeni, nikawaambia sihongeki, wananchi wangu wamejipanga na kunichangua ili niwaletee maji, Namanyere hawana maji kwa ajili ya tamaa za watu."

Kessy alisema mradi wa Bwawa la Fili ambalo gharama zake zilionesha kuwa ni Sh. milioni 900 wakati uhalisia ni Sh. milioni 300.

Kessy akionyesha kukerwa na hali hiyo, alisema kwenye mradi wa maji wa Kilando, mkandarasi alilipwa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kujenga vizimba 18 wakitumia mifuko 5 ya saruji kwa kila kizimba na kuwa hakuna kilichofanyika katika mradi huo.

"Tulimwambia Waziri aliyepita (bila kumtaja jina) mbele ya bwawa pamoja na aliyekuwa RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) ambaye sasa ni Katibu Wizara ya Tamisemi, kuwa wasimlipe mkandarasai hizo Sh. milioni 300 zilizobaki mpaka wajiridhishe, lakini walimlipa kama mkandarasi yupo hajafa basi azitapike hizo hela.

Kessy alieleza masikitiko yake akisema: "Watu wanakaa ofisini na kutunga gharama za maji, mfano kule kwangu (Nkasi), mtaalamu anasema gari lilitoka Dar hadi Namanyere kwa shilingi milioni 12, niliwaambia naombeni risiti, hakuna, mabomba yaliyoletwa hakuna, nipeni namba ya gari sikupewa na hata nilipokwenda Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) hakuna kilichofanyika.

Mbunge huyo ameeleza kuwa yuko Waziri mmoja akimtaja ni aibu, na alipomwambia kuhusu ubadhirifu wa maji katika eneo lake alimjibu utajuaje masuala ya utaalamu na yeye akamwambia nitakushitaki kwa Rais, akatetemeka.

"Naweza kumtaja mimi, Waziri huyo alinitishia humu bungeni, wewe mzee hata kipofu anajua. Waziri anashirikiana na mafisadi, hufai kuwa Waziri wewe utumbuliwe," alieleza Kessy

Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, alisema bado kuna tatizo la usimamizi kwenye wizara hiyo kususani katika mamlaka za maji.

Alisema ni muhimu hatua za maboresho zikafanyika kama ambavyo Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Dar es Salaam (DAWASA) ilivyoweza kubadili utendajikazi wake.

Kadhalika alisema hoja ya kuongezwa tozo ya Sh. 50 kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Maji, sasa ni muda mwafaka ukazingatiwa.

Naye, Mbunge wa Madaba (CCM), Joseph Mhagama, aliieeza kuna haja ya kuwachukulia hatua watumishi wa wizara hiyo ambao hawataki kubadilika.

Mbunge wa Muheza (CCM), Adadi Rajabu, alisema kuwa kwenye jimbo lake kuna mradi ambao unatoa maji kutoka Pongwe hadi Muheza na ili kuondoa tatizo la maji kwenye jimbo hilo ambao ulitegemewa kumalizika Mei mwaka jana, hadi sasa bado unaendelea kujengwa na umefikia asilimia 70.

"Kazi kubwa inafanyika, lakini mradi huu ambao tunautegemea ulikuwa kwenye mpango huo ili kupunguza tatizo la maji Muheza. Sasa hivi kama nilivyosema imebaki kitu kidogo kwa asilimia 30 ili maji yatiririke Muheza ingawaje haitakidhi sehemu kubwa,"alisema

Balozi Adadi ameeleza kuwa, "Kwenye bajeti nimeona imepangwa zaidi ya milioni 700, namuomba Waziri aruhusu wakati mradi mkubwa unasubiriwa mabomba hayo yaanze kufumuliwa ili mkandarasi aanze kazi na maji yapatikane wakati wanasubiri mradi hu mkubwa.

Kuhusu mradi wa India wa dola milioni 500 ambao alisema ni muhimu na unachukua eneo kubwa la miji karibu 29 nchini na kwamba utakapoanza au kukamilika utapunguza kasi ya maji.

Mbunge wa Handeni (CCM) Mboni Muhita, aliitaka serikali kuunda tume ya uchunguzi kwenye miradi ya mabwawa kwani fedha nyingi zimeibiwa.

"Serikali ichunguze ubadhirifu kwenye miradi ya mabwawa ya Manga, Makata na Kwandumbwa ambapo zaidi ya bilioni moja zimeliwa. Fedha zile zinapaswa zitapikwe kwani licha ya baadhi ya wakandarasi kushikiliwa lakini hakujamaliza changamoto ya maji," alibainisha



### MTAMBO KUSAFISHA MAJI TAKA JANGWANI

Akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20, Waziri Profesa Mbarawa alisema serikali itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya uondoaji majitaka kwa kushirikiana na serikali ya Korea Kusini, utakaogharimu dola za Marekani milioni 90.

Wizara hiyo inaomba kuidhinishiwa na Bunge, bajeti ya jumla ya Sh.634, 196,197,530 kwa ajili ya mwaka 2019/20.

Alisema hadi kufikia Aprili mwaka huu, mtaalamu mshauri atakayesimamia mradi huo amepatikana na ameanza kazi ya mapitio ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni.

"Mradi huu utahusisha ujenzi wa mfumo wa majitaka wa mabomba yenye urefu wa kilometa 376 kutoka maeneo ya katikati ya Jiji, Ubungo, Kinondoni, Mwananyamala, Msasani na Ilala hadi kwenye mtambo wa kusafisha majitaka utakaojengwa eneo la Jangwani," alisema Profesa Mbarawa (Pichani).

Prof. Mbarawa ameeleza kuwa mtambo huo utakuwa na uwezo wa kusafisha lita milioni 200 za majitaka kwa siku.

Akiwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Msemaji wa kambi hiyo katika Wizara ya Maji, Devotha Minja (Viti Maalum-Chadema), alisema katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji ni lazima kuifanya rasilimali hiyo kutumika kwa uangalifu na uendelevu baina ya makundi yote ya jamii.

Alisema kambi hiyo inaishauri serikali ni muhimu mahitaji ya maji katika kila kundi kwenye mfumo wa uzalishaji ijulikane mahitaji yake ili kuweza kupanga mgawanyo rasilimali hiyo endelevu.

Pia, akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mahmoud Mgimwa, alisema ni muhimu ushauri huo uliotolewa kwa miaka mitatu mfululizo ukazingatiwa.

"Kwa miaka mitatu sasa kamati imekuwa ikiishauri serikali kuimarisha makusanyo ya Mfuko wa Taifa wa Maji kwa kuongeza tozo ya mafuta kwa kila lita ya petroli na diseli kutoka Sh. 50 hadi Sh. 100.

## JPM afichua bunduki

INATOKA UK. 5

nimetoa, isije ikawa zimerudi tena kwa wawekezaji au wamekuja wengine wapya kisirisiri.

"Lengo la yale mashamba yalikuwa si kupewa wawekezaji tena, lengo lilikuwa ni kupewa wananchi kwa ajili ya kulima," Rais Mgufuli alisema.

Kiongozi huyo wa nchi pia aliagiza kutafutwa madalali ambao wamekuwa wakiwawakodishia wananachi mashamba kwa kiwango kikubwa cha fedha ili kulima.

"Mwekezaji wa shamba namba 70 na 78 alipewa kihalali kwa mujibu wa sheria, na alipokuwa na shamba lake amekuwa akilima lakini katika maeneo mengine amekuwa akiwapa watu kwa kuwakodisha, lakini kwa bahati mbaya kuna madalali hapa katikati wamekuwa wakiuza kwa kukodisha kwa Sh. 600,000 mpaka Sh. 700,000, ninaomba watafutwe," aliagiza.

Kabla ya kuhutubia katika viwanja vya Rujewa, Rais Magufuli alisimama mara kwa mara njiani kwa ajili ya kusikiliza kero na kuzungumza na wananchi, akitoa onyo kwa watumishi wasio waamifu ambao wamekuwa wakipewa kusimamia miradi ya serikali na kuiba pesa za serikali.

Rais Magufuli pia alitoa wito kwa watendaji wa serikali kuhakikisha wanashughulikia matatizo ya wananchi kwa haraka.

## ...Bunge lazizima

INATOKA UK. 2

anakumbuka yale makundi ambayo yako magnalized (maalumu) kwa mfano watu wenye ulemavu, watu wanaoishi kwenye mazingira magumu, albino na kawaida namna alivyowasaidia na kuwapigania.

**OWENYA**

Pia, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa Kilimanjaro (Chadema), Lucy Owenya, akizungumzia namna alivyopata taarifa za kifo chake alisema, "nimepokea kwa masikitiko sana kifo cha Dk. Reginald Mengi, mimi namuita kaka yangu, kwanza kwenye community (jumuiya) ya wafanyabiashara tumempoteza mtu muhimu sana kwa sababu tulikuwa tukiona jinsi alivyokuwa anatupigania katika mambo ya kibiashara, sio hilo tu alikuwa mtu wa watu, kama taifa tumepoteza nguzo muhimu sana."

**HAULE**

Mbunge wa Mikumi (Chadema), Joseph Haule, akizungumzia msiba huo, alisema umemshtua kwa sababu alikutana naye siku si nyingi, ni mtu pekee aliyewavutia vijana wakati wa uhai wake akiwasihi kupambana na kuwataka wasikate tamaa katika uongozi na utafutaji.

Alisema kauli yake ya kutotaka watu wasikate tamaa amekuwa akiitumia mara nyingi na hata kitabu chake cha 'I can, I must, I will' aliitumia katika nyimbo yake kuwapa moyo Watanzania.

## HABARI KITAIFA

# Fisi washambulia watu, mifugo vijijini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

IMEIBUKA hofu miongoni mwa wananchi wa kata za Kilago na Nyandekwa katika Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, baada ya makundi ya wanyama wakali wanaodhaniwa kuwa ni fisi kuingi katika makazi yao na kushambulia watu na mifugo.

Usiku wa kuamkia Aprili 29, mwaka huu yaliibuka makundi ya fisi katika kata hizo na kujeruhi watu watano waliokimbizwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, huku wanyama hao wakiua mbuzi watano.

Diwani wa Kilago, Peter Emmanuel, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa licha ya kujeruhi watu, wananchi walijitokeza kwa wingi kutoa msaada, na katika purukushani wananchi hao waliua fisi mmoja.

Alisema makundi ya wanyama wameingia katika vijiji mbalimbali vya kata yake kwa lengo la kula mifugo kama kuku, mbuzi na ng'ombe, na kuongeza kuwa wakati mwingine wanyama hao wanaingia kijijini nyakati za mchana.

"Kwa nyakati za mchana tunahofia watoto wetu ambao wanasoma katika shule ambazo zipo mbali na kijiji," alisema diwani huyo na kuongeza: "Nashangaa kuona ongezeko la wanyama hao kwa kuwa licha ya uwapo wa mapori katika maeneo yetu hawajawahi kuja na hasira kama hizi pengine wameongezeka. Naomba mamlaka inayohusika na wanyamapori isaidie wananchi kwa kuwalinda."

"Ikiwezekana wawawinde ili wawahamishie huko katika mapori, kwa hali kama hii hatutaweza kwenda katika mashamba ya mpunga kwa kuwa huku nyuma watatafunа mifugo pamoja na watoto wetu," alilieleza Emmanuel.

Aliishauri idara ya wanyamapori kuhakikisha inafanya zoezi la kuwawinda wanyama hao ili kunusuru maisha ya wananchi wa kata hizo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. Lucas David, alikiri kuwapokea majeruhi watano walioshambuliwa na fisi na kuongeza kuwa walipatiwa matibabu ya haraka, ambapo jopo la madaktari walipambana katika kuokoa uhai wao.

"Ni kweli wananchi watano kutoka Kata ya Kilago walilazwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama kwa ajili ya kupatiwa matibabu... kwa kweli jopo la wataalamu wangu lilishughulika vilivyo na kuokoa maisha yao na baada ya hali zao kuwa nzuri waliruhusiwa," alisema Dk. Lucas David.

Diwani wa Kata ya Nyihogo, Shadrack Mgwami, alisema licha ya fisi, pia kuna mbwa ambao wanazagaa katika maeneo mbalimbali ya viunga vya Mji wa Kahama ikiwamo hospitali ya Kahama Mji, na kwamba anahofia wana kichaa na iwapo watang'ata watoto wa shule gharama ya kuwatibu itakuwa kubwa.

Afisa Maliasili na Wanyamapori wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Thomas Manumbu, alithibitisha kuwapo kwa matukio hayo, na kusema tatizo la fisi kuvamia makazi ya wananchi katika Halmashauri hiyo ni kubwa, na kutaja kata za Kilago, Nyandekwa na maeneo ya kijiji cha Kakebe.



Katibu Tawala wa wilaya ya Arumeru, Mwl. Jemsi Mchembe, akiongea na wananchi wakati wa uzinduzi wa ofisi ya kijiji ya Songoro, iliyojegwa kwa nguvu ya wananchi, wilayani humo juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Madereva sasa waimarishiwa usalama

**Na Elizabeth Zaya**

MADEREVA wamekumbikwa, baada ya kuzindiliwa kitufe cha dharura (SOS) kwa lengo la kuimarisha usalama wao wanapokutana na hatari yoyote.

Kitufe hiyokimezinduliwa na Kampuni inayotoa huduma za usafiri kwa njia ya mtandaoni nchini - Bolt

Akizungunza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa Bolt Tanzania, Remmy Eseka, alisema madereva wanaotumia programu hiyo ya Bolt sasa wanaweza kutumia huduma hiyo mpya ya usalama muda wowote watakapohisi kuwa wapo hatarini au eneo ambalo si salama.

Alisema matumizi hayo ya kitufe cha dharura dharura yamekuwa kama muendelezo wa Bolt kutumia teknolojia kuimarisha usalama wa madereva wanapokuwa barabarani.

"Usalama wa dereva na abiria ni swala la muhimu sana kwetu. Tunaongeza safu ya usalama wa dereva zaidi ya ule uliopo tayari wa kufutalia mubashara safari kwa kutumia GPS na mfumo wa thathmini.

"Kitufe cha dharura kilichopo kwenye programu ya Bolt ya dereva, huwezesha taarifa kuwafikia kampuni ya ulinzi ya SGA Tanzania," alisema meneja kampuni hiyo.

Meneja wa mauzo na masoko kutoka SGA, Faustina Shoo, alisema kitufe cha dharura kilichowekwa kwenye programu ya madereva kinapotumika, simu hupelekwa kwenye kituo cha dharura cha SGA, ambao baada ya kuhakiki uhalali wa dereva, wanapeleka gari la wagonjwa au timu ya askari kuelekea alipo dereva kumsaidia kama watoa huduma wa kwanza.

"Bolt italipia gharama hizi pamoja na gharama zitakazo pitishwa kwa kila tukio. Tunaendeleza nia yetu ya kujibu mahitaji ya wateja/wabia kwa kutoa huduma ya uokoaji wa dharura kwa madereva wa Bolt kutokana na ubia huu.

"Madereva wa Bolt wanahakikishiwa kupata huduma ya saa 24 kupitia kitengo chetu cha dharura iwapo watapata tatizo wakiwa safarini." alisema.

## DC asisitiza ulipaji kodi kumuunga mkono JPM

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa wilaya ya Kahama, Annamlingi Macha, amewataka wananchi kulipa kodi ya majengo kumuunga mkono Rais John Magufuli katika mkakati wa utegemezi wa fedha za wafadhili.

Amesema kulipa kodi za serikali ikiwamo hiyo, kutaiwezesha nchi kujitegemea na kuiletea heshima kimataifa.

Aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa kampeni ya usajili na ulipaji kodi ya majengo katika mji mdogo wa Kakola katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, aliwataka wananchi kuwa wazalendo na kushiriki katika ujenzi wa taifa kwa kuchangia kupitia kulipaji kodi ya majengo.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wengine, Dubbey Erassy, aliitaka serikali kurasimisha maeneo yao kabla ya kuanza kutoza kodi hiyo, hali itakayowawezesha kukopesheka kwenye taasisi za fedha.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa wa kikodi wa Kahama, Warioba Kanile, alisema shughuli za mamlaka hiyo ni kusajili, kukadiria na kukusanya fedha za serikali ambazo baadaye zinaenda kwenye utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Afisa elimu kwa walipakodi Mkoa wa Shinyanga, Anthony Faustine, aliwataka wananchi kudai risiti wanaponunua bidhaa na huduma, vinginevyo ni ukiukwaji wa sheria ya ulipwaji kodi. Mwananchi mwingine, Isaya Phillemon, alisema pamoja na kukubali kulipa kodi hiyo, wametaka serikali kuendelea kutoa elimu kutokana na tozo za kodi zinazotokana na wizara mbalimbali ikiwamo ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya Fedha na Mipango.

DC Macha alisema kulipa kodi ni suala la kisheria na haitozwi ovyo ovyo na ili itozwe lazima iwekwe sheria na ipitishwe kwenye mchakato wa bunge, na kwamba kuhimiza kulipa kodi ni kuhimiza uzalendo na maendeleo ya nchi.

"Mambo yanayofanywa na serikali ya Rais John Magufuli ya maendeleo ni makubwa. Watanzania tumeomba misaada vya kutosha, tutumie rasilimali zetu na kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo yetu, "alisema Macha.

## Makazi 4,700 yarasimishwa

SERIKALI imesema mpaka sasa, makazi 4,768 yamerasimishwa wilayani Muheza mkoani Tanga.

Vilevile, serikali itaendelea kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi, kurasimisha makazi, kupima viwanja na mashamba ili kumaliza migogoro ya ardhi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Yosepher Komba (Chadema).

Mbunge huyo alisema kuna uhaba wa watumishi na vitendea kazi katika Idara ya Ardhi na Maliasili wilayani Muheza unaosababisha kuazima watumishi na vifaa kutoka halmashauri nyingine.

"Je, ni lini serikali itaajiri watumishi na kununua vitendea kazi katika idara hiyo na je, serikali iko tayari kuwawekea wananchi wanasheria ili kusaidia kutatua migogoro ya ardhi," mbunge alihoji.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema Idara ya Ardhi na Maliasili katika halmashauri hiyo Muheza inao watumishi 12 kati ya 20 wanaohitajika.

Alisema halmashauri imeendelea kuomba vibali kwa ajili ya kuajiri watumishi hao na hata hivyo ili kukabiliana na upungufu huo halmashauri imeajiri watumishi watatu wa ardhi kwa mkataba ili kutatua changamoto mbalimbali za ardhi.

"Vilevile, katika mwaka wa fedha 2017/18, kupitia mapato yake ya ndani, halmashauri ilinunua GPS-RTK kwa kwa ajili ya upimaji ardhi gharama ya Sh. milioni 37," alisema.

Waitara aliongeza kuwa halmashauri imetoa gari aina ya Toyota Land Cruiser kwa ajili ya Idara ya Ardhi na Maliasili na halmashauri itaendelea kununua vitendea kazi kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha.

Alisema serikali inao mfumo wa kisheria wa utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye mamlaka za serikali za mitaa ambao umeainishwa katika Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2002 na kanuni zake.

"Migogoro ya ardhi iliyoko Wilaya ya Muheza imegawanyika kwenye makundi makuu matatu, migogoro ya kiwilaya ambayo inahusisha mipaka ya vijiji vya Wilaya ya Muheza na Tanga Jiji pamoja na vijiji vya Muheza na Pangani," alibainisha.

Waitara alisema migogoro hiyo inashughulikiwa katika ngazi ya mkoa na itapatiwa ufumbuzi wakati wowote sambamba na migogoro ya mipaka na vijiji iliyotokana na upimaji wa mipaka nchi nzima uliofanyika mwaka 2007.

"Vikao kwa ajili ya kumaliza migogoro hii vinandelea na vimefikia hatua nzuri, migogoro mingine ni migogoro ya viwanja ambavyo hupokewa na kutatuliwa kwa utaratibu wa kawaida na mamlaka za serikali za mitaa," alisema.

Sambamba na hilo, alisema suluhisho la kudumu kwa aina hiyo ya migogoro ni kukamilisha mpango wa matumizi bora ya ardhi, kupima viwanja na kurasimisha makazi,

# Hospitali ya wilaya inahifadhi maiti moja

BUNGE limeelezwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kilwa ina jokofu moja lenye uwezo wa kuhifadhi maiti moja lilonunuliwa mwaka 1996.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, alibainisha changamoto hiyo alipojibu swali la Mbunge wa Kilwa Kusini (CUF), Selemani Bungara.

Mbunge huyo alisema hospitali hiyo haina jokofu la kuhifadhi maiti na majengo yake mengi ni chakavu.

"Je, serikali ina mpango gani wa kununua jokofu jipya sambamba na kukarabati majengo ya hospitali hiyo?" Bungara alihoji. Akijibu swali hilo, Kandege alisema kutokana na hali hiyo, serikali inaendelea na taratibu za kukamilisha hatua za kuanza ujenzi wa jengo jipya la kuhifadhi maiti kwenye hospitali hiyo sambamba na ununuzi wa jokofu jipya la kisasa. Alisema serikali itaendelea kukarabati miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Alisema hospitali hiyo ni miongoni mwa hospitali kongwe za wilaya nchini na imekuwapo tangu mwaka 1965.

"Kwa kutambua umuhimu wa hospitali hiyo, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekuwa ikifanya ukarabati na upanuzi wa majengo mbalimbali ya kutolea huduma," alisema.

Alibainisha mwaka wa fedha 1996/07 ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya hospitali ulifanyika sambamba na ujenzi wa kliniki ya mama na mtoto. "Mwaka 2010, ulifanyika ujenzi wa jengo la huduma za Ukimwi (CTC), mwaka 2012, ulifanyika ujenzi wa jengo la wazazi na mwaka 2017, ulifanyika ujenzi wa jengo la mama ngojea," alisema.



Baadhi ya wadau wa habari, wahariri na waandishi wa habari, wakiwa kwenye mkutano wa Maadhimisho ya Wiki ya Uhuru wa Habari, yaliyofanyika, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polisi wawanunulia chakula mahabusu

MBUNGE wa Masasi, Rashid Chuachua (CCM), amesema Jeshi la Polisi wilayani Masasi mkoani Mtwara, linafanya kazi katika mazingira magumu huku askari wakilazimika kutoa fedha zao mfukoni kuwanunulia chakula mahabusi.

Mbunge huyo alitoa kauli hiyo bungeni jana wakati wa kipindi cha 'Maswali', akieleza jeshi hilo linafanya kazi kwenye mazingira magumu kutokana na uchakavu wa miundombinu na uhaba wa vitendea kazi.

"Je, ni lini serikali itawapatia magari askari polisi wa Wilaya ya Masasi kutokana na kutokuwa na magari ya kutosha? Je, ni lini serikali itajenga nyumba za askari katika Wilaya ya Masasi?" mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema serikali inatambua uhaba wa vitendea kazi kwa jeshi hilo ikiwa ni pamoja na uchache wa magari.


"Kwa sasa, Wilaya ya Masasi imeshapatiwa gari moja aina ya Leyland Shok, hivyo kufanya kuwapo kwa magari matatu ambayo ni PT 1865 Toyota Landcruiser, PT 4011 Grand Toger na Leyland Ashock," alisema.

Aliongeza kuwa gari hilo jipya linatumika kwa shughuli mbalimbali kama doria na operesheni kubwa na kutokana na jiografia Wilaya ya Masasi na jeshi hilo litaiongeza wilaya hiyo magari kwa kadri yatakavyopatikana.

Hata hivyo, Masauni alisema hakuna utaratibu wa askari polisi kutoa fedha zao mfukoni kwa ajili ya chakula cha mahabusi, akieleza kuwa utaratibu uliopo ni serikali kupitia jeshi hilo lina wajibu wa kuwapatia chakula mahabusu waliopo korokoroni.

Alisema ndugu za mahabusu pia wanaruhusiwa kuwapelekea chakula jamaa zao walioko mahabusi. Pamoja na hayo, alisema wilaya hiyo ina nyumba za makazi ya askari zipatazo 15 ambazo zinatumiwa na familia za askari 30.

"Ingawa ni kweli askari wengine wapatao 154 bado wanaishi uraiani, serikali itaendelea kujenga nyumba za makazi ya askari kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



Mwenyekiti wa Chama cha Makatibu Muhtasi Tanzania (TAPSEA), Zuhura Maganga (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Arusha jana, akitoa ombi kwa Rais John Magufuli, kusaidia chama hicho, kuwabana waajiri wanaowanyima fursa wenzao ya kushiriki mikutano ya chama hicho na kwenda kujiendeleza. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Makatibu Mahsusi wamwomba JPM kuwabana waajiri

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA cha Makatibu Mahsusi (TAPSEA), kimemwomba Rais John Magufuli, kusaidia kwa kuwabana baadhi ya waajiri nchini wanaodharau chama hicho na kuwanyima fursa ya masomo na kushiriki mikutano ya wanachama wenzao.

Akitoa ombi hilo jana jijini Arusha, Mwenyekiti wa chama hicho, Zuhura Maganga, wakati akiongea na waandishi wa habari, alisema suala la badhi ya waajiri limekuwa kero kwao na linarudisha nyuma jitihada za chama kuendeleza wenzao.

"Sasa hili tatizo sababu huyu Katibu Mahsusi anapoenda kusoma anaendana na changamoto za kiteknolojia zinazojitokeza sababu anapanua wigo wa uelewa," alisema.

Alisema ni vema sasa Rais Magufuli akaliingilia kati na kueleza waajiri hao kinachopaswa kufanywa kwao, kwa kuwa chama hicho kipo kihalali na kimesajiliwa tangu mwaka 2008 na kuzinduliwa rasmi 2012.

Zuhura alisema katika mkutano wao wa washiriki zaidi ya 2,300 wa Tanzania Bara na Visiwani, ulioanza jana unatarajiwa kufunguliwa leo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika.

Alisema katika mkutano huo watajadili mada mbalimbali ikiwamo utunzaji wa siri na uzalendo katika taifa, matumizi ya muda wa kazi ili kuleta tija na ufanisi, haki za binadamu na utawala bora.

Alisema kaulimbiu ya mkutano huo ni "Tumia muda wako vizuri kufanya kazi ili kuongeza ufanisi na tija".

Pia aliomba waajiri watoe vipaumbele kwa Makatibu Mahsusi kwenye shughuli zao, ili waonyeshe ujuzi wao ikiwamo kupandishwa vyeo.

Alisema mbali na mada hizo kutolewa pia watajitolea damu salama kwa ajili ya kusaidia wahitaji na zoezi hilo ni endelevu kwao kwa kila mkutano wanaofanya.

Naye Katibu wa chama hicho, Anneth Mwapima, alisisitiza kuwa katibu mahsusi ni mtu muhimu katika serikali au taasisi yoyote, kwa kuwa yeye ndio anatunza siri za serikali na taasisi.

Pia alisema wananchi ni vema wakapuuza upotoshaji wa kuwa fani hiyo ya wanawake pekee, kwasababu wapo wanaume zaidi ya 10 wanafanya kazi vizuri.

# Waandamana kupinga kuchukuliwa chanzo cha maji

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya wananchi 45,000 katika kata tano za Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, wameandamana hadi Kijiji cha Shiboro, Kata ya Sambasha, kupinga halmashauri hiyo, kuchukua chanzo cha maji cha Ngarenarok, bila ya kushirikisha wananchi wa maeneo hayo.

Wakizungumza jana kwa niaba ya wananchi wengine, wakati wa maandamano hayo, John Lukumayi na Grace Julius, walisema kitendo cha halmashauri hiyo, kuchukua chanzo hicho kitawasababishia wananchi hali ya ugumu wa maisha.

"Chanzo hiki cha maji tunakitegemea katika hatua ya kujikimu kimaisha, kusomesha watoto, kujenga nyumba, kumwagilia mazao, matumizi ya majumbani na kulipia kodi za nyumba, lakini tutaponyang'anywa hali zetu kimaisha zitakuwa ngumu," alisema Lukumayi.

Wananchi hao, wamemuomba Waziri wa Maji, kuingilia kati mgogoro huo, kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi kwa kuwa njia zote walizotumia kumaliza changamoto hiyo haikufanikiwa.

Mwenyekiti wa chanzo cha maji (Mfereji wa Masaga), katika Kijiji cha Shiboro, George Mollel, alisema kuchukuliwa kwa chanzo hicho, kimewaathiri wananchi wa maeneo hayo, kwa kuwa wanakitegemea kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kumwagilia mashamba.

"Mwaka 1998 baada mvua za El-nino maji yalipungua kwenye chanzo hiki na tulipofuatilia kwenye chanzo kikuu huko Mlima Meru, tulibaini kuwa chanzo kimoja kilishachukuliwa na serikali na kuingizwa katika mfumo wa maji ya kulipiwa," alisema Mollel.

Alisema baada ya kubaini kuwa serikali walishachukua chanzo, wananchi kwa pamoja walikubaliana wasifuatilie tena, lakini wavilinde vyanzo vya maji ambavyo wamebakiwa navyo.

"Baada ya hapo tuliitisha mkutano kuweka utaratibu wa kusajili maji hayo, kwa ajili ya kutumiwa kisheria na tulipewa kibali na serikali cha kutumia," alisema.

Alisema Mwaka 2003, walianza kulipia maji hayo Sh.70,000 kwa mwaka na baada ya kupita miaka mitano, bei ya kulipia maji iliongezeka hadi kufikia Sh. 100,000 kwa mwaka.

"Mwaka 2015, watu kutoka vijiji vya Lemong'o (Kata ya Oldonyosambu) na Lenjani (Kata ya Lemanyata), walileta maombi kwenye Ofisi ya Kijiji kuomba maji hayo, lakini hawakufuata utaratibu na hatukushirikishwa kitu chochote na tunaona dalili za kuchukuliwa kwa maji haya bila ya maridhiano yoyote," alisema Mollel.

Ofisa Tawala wa Wilaya ya Arumeru, Magret Mwishashu, alisema katika hatua ya kushughulikia suala hilo, Mwenyekiti wa kijiji hicho na uongozi wa chanzo hicho cha maji walifika katika Ofisi ya Mkuu wa wilaya, lakini hawakufanikiwa kumuona kutokana na majukumu ya kikazi.

# RC Arusha afungua soko la madini Longido

**Zanura Mollel,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amefungua soko la madini katika Kata ya Namanaga, wilayani Longido na kuwataka wafanyabiashara kulitumia ipasavyo.

Gambo alisema uwapo wa soko hilo ni kuhakikisha usalama kwa wafanyabiashara wa madini upo, hivyo wasiwe na shaka kuhusu biashara yao.

Alidai kuwa eneo hilo ni la mpakani wanaingia mataifa mbalimbali, hivyo kuwataka wote watakao jihusisha na biashara ya madini nje ya nchi kuhakikisha wanakuwa na hati ya kusafiria ili kuepusha usumbufu.

"Soko hili lina eneo maalum kwa ajili ya kuhifadhi madini, pale inapotokea mfanyabiashara anahitaji kuhifadhi kutokana na usalama wa mali yake, hivyo ni imani yangu wataitumia fursa hiyo ipasavyo," alisema.

Pia alisema soko hilo litasaidia kupunguza utoroshaji wa madini na utapeli kwa watu wasio na nia njema.

Alisema kwa wafanyabiashara wanaodai nchi jirani ya Kenya ina madini mapya aina ya Rubi, ukweli ni kwamba madini hayo yanapatikana Tanzania.

"Hii ilitokana na ukosefu wa eneo maalum ya uuzaji wa madini, ila kwa sasa hali ya ujanja ujanja itapotea," alisema Gambo.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema soko hilo si la wilaya pekee bali ni soko la mkoa kwa ajili ya madini na kuwataka wafanyabiashara kufanyabiashara kwa kufuata taratibu na sheria za nchi.

Alisema uwapo wa soko hilo utapunguza kero mbalimbali za wafanyabiashara na kuwa soko hilo sio la maigizo kwa kuwa limeanza kazi rasmi na kila mmoja wa sekta hizo alitumie kwa maslahi ya nchi na mapato binafsi.

Mmoja wa wachimbaji, Rahim Mollel, mmiliki wa mgodi wa Mundarara Rubi Mining (AIKATAI), alisema kuwapo kwa soko hilo kutasaidia upatikanaji wa wanunuzi kutoka mataifa mbalimbali na uuzaji wa madini kiusalama zaidi ya zamani.

Alisema katika mgodi wake anazalisha madini aina tatu, ambayo ni Rubi Block, Zozaiti na Caption na huuzwa kwa tani, kilogramu na gramu.

Akitoa ufafanuzi wa uuzaji wa madini hayo kwa njia ya viroba, alisema madini wanayoyauza kwa viroba, baada ya Tume ya Madini kukamilisha uthaminishaji ni aina ya Caption.

" Tunayaweka kwenye viroba, tunawauzia wananchi na wao wanaenda kuchakata wapate ridhiki na kujiinua kiuchumi," alisema.

Naye Kaimu Ofisa Madini Mkoa, Robert Eric, alisema soko hilo linatambulika kisheria na sasa wachimbaji watasimamiwa na kupata soko na kuondokana na utapeli waliokuwa wakifanyiwa katika kutafuta soko.

Soko hilo litajishughulisha na uthaminishaji wa madini na taratibu zote zitapatikana ndani ya soko pamoja na kujua aina ya madini, kujua kiasi, thamani na kuuza.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Arusha (TRA), Faustine Mdessa, aliwataka wanaotaka kufanyabiashara ya madini, kupita TRA ili wapate usajili, wawe wafanyabiashara halali wa madini na kuwataka kutoshauriwa wala kushawishiwa na watu wenye nia mbaya na usajili ni bure.

Alisema kuwa kulikuwa na malalamiko ya kodi ya zuio asilimia tano kwa madini yanayo kwenda nje ya nchi kuanzia Februari 22, kodi hiyo imefutwa, ili kila mtua afuate sheria.





# Waiomba wizara kutupia macho hospitali zinazolalamikiwa

Na Mary Mosha, MOSHI

BAADHI ya wagonjwa wanaopata matibabu katika Hospitali ya Rufani KCMC, wamemuomba Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kuitazama upya hospitali hiyo kwa kile walichodai manyanyaso kwa wagonjwa na lugha chafu kutoka kwa watumishi hasa kitengo cha uhasibu.

Walitoa maoni hayo siku moja baada ya gazeti hili kuripoti shutuma zilizotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, katika sherehe za wafanyakazi (Mei Mosi) kuhusu huduma mbovu na manyanyaso katika hospitali hiyo na Mawenzi.

Akitoa malalamiko yake, Elias Mpingo, alisema kuwa ipo haja kwa serikali kuangalia namna ya kudhibiti watendaji katika sekta binafsi hasa za afya kutokana na watendaji hao kujiona miungu watu kwenye taasisi walizopo.

"Mimi nimelazwa hapa na mwanangu kwa takribani mwezi mmoja sasa, majibu ninayoyapokea mara kwa mara kutoka kwa wauguzi ni kufedhehesha na kukatisha tamaa.. Waziri kama unatusikia tunaomba uchukue hatua stahiki ili kuokoa uhai wa Watanzania maskini kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini," alisema.

Enock Sabastian alisema: "Nimefika hapo wiki tatu mwanagu aliungua, lakini sijapata matibabu stahiki zaidi ya jopo la madaktari wanafunzi kufika na kufanya kazi zao bila huduma inayoeleweka."

"Hawa wanafunzi madaktari wamekuwa wakifika na kumfanyia mwanangu majaribio kila mara bila kuongea na mimi chochote huku wakitumia lugha ya Kiingereza ambayo kwa kweli siifahamu...hii inaumiza sana na kwa sasa nimekata tamaa mwanangu kupona, nasubiria kuona kifo chake tu," alisema. Hance Samweli, alisema watendaji hao pamoja na uongozi wao hawana muda wa kutoa elimu wala kuwasikiliza wagonjwa na badala yake hutoa majibu machafu kisha kuondoka.

"Mimi mwanangu alitakiwa kufanyiwa operesheni ya nyama za pua toka Aprili 2018, lakini ninapigwa kalenda kila siku na baada ya kufuata uongozi waliniambia kama naona nateseka nikamtibu mwenyewe mwanangu nyumbani kwa kuwa wagonjwa wapo wengi watakuja," alidai huku machozi ya kimtoka.

"Lakini wapo wenzangu wamekuja hapa na wanafanyiwa upasuaji na kwenda zao hii wanaonyesha ubaguzi wa hali ya juu na tunaomba serikali kwa ngazi zote kuchukua hatua stahiki ili kutokomeza tabia hii," alisema Hance. Mkurugenzi Mtendaji wa KCMC, Gileard Masenga, alipotafutwa na mwandishi wa Nipashe, kujibu tuhuma hizo, alisema hawezi kuongea kwa sasa.

Aidha, ilipowasiliana na Meneja mauzo wa hospitali hiyo, aliyetambulika kwa jina moja la Evelyne, alimjibu mwandishi kuwa hawako tayari kuzungumzia suala hilo.



Kijana akitoka kukata majani kwaajili ya kulisha mifugo, katika eneo la Uwanja wa Taifa, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima mpunga Hai wapewa somo

Na Mary Mosha, HAI

WAKULIMA wa mpunga wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, wametakiwa kufuata ushauri wa kitaalamu katika kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo.

Nsajigwa Ndagile, Ofisa Tarafa Masama, akizungumza na viongozi mbalimbali wakiwamo wa vijiji vya Chekimaji, Kawaya na Mkarama, alisema mpunga ni zao la pili la chakula likitanguliwa na mahindi, lakini iwapo wakulima watazingatia ushauri wa wataalamu hao mavuno ya zao hilo yataongezeka.

"Wakulima hao wamekuwa wakilima bila kufuata utaratibu wa wataalamu mwisho wa siku wanapata mazao kidogo hivyo kupata hasara jambo ambalo linarudisha maendeleo nyuma," alisema.

Aidha, aliwataka wakulima hao kutumia maji kwa zamu ili kupunguza mgogoro katika eneo hilo unaofukuta kwa muda na kutishia kuzuka mapigano kati ya wakulima wa mpunga na wa mazao ya mboga.

Ofisa umwagiliaji wa eneo hilo, Adolph Mboya, aliwataka wakulima hao kuzingatia hatua tano ambazo zipo kisheria ili kulinda mfereji huo usikauke pia amewataka wakulima hao kupunguza ukubwa wa mashamba kutokana na maji kupungua katika mfereji huo wenye matawi 11 ambayo ni rasmi na michipuo zaidi 30 ambayo sio rasmi. Ofisa huyo alisema kuwa watafanya mikutano kuwafahamisha wakulima hao umuhimu wa kulinda mazingira kwa kuacha hatua tano pia kuacha kuchukua maji kwenye mfereji huo bila kufuata utaratibu unaotakiwa kwa kuwa ndiyo mwanzo wa kugombea maji kutokana na sehemu nyingine kutofika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Cheki maji, Suleimani Juma, amemshukuru Ofisa huyo kufika katika eneo hilo na kuzungumza namna ya kumaliza mgogoro huo kutokana na mtu mmoja kujeruhiwa hivi karibuni wakati akigombea maji.

Wakulima zaidi ya 500 wananufaika na kilimo cha umwagiliaji katika eneo hilo.

# Jamii yatakiwa kuanzisha mfuko wa maafa

Na Mary Mosha, MOSHI

JAMII imetakiwa kuwa na mfuko maalumu wa maafa ndani ya kata na kuwa na utaratibu wa kusaidiana inapotokea janga au majanga kama ya kuunguliwa nyumba, mafuriko pamoja na magonjwa ya milipuko.

Ushauri huo ulitolewa na Makamu Mwenyekiti wa Muungano wa vyama vya Ushirika ya Uru Kaskazini, Felix Masao, wakati akikabidhi mabati 20 kwa Deogratias Urio, ambaye ni mwanachama wa Chama cha Ushirika Uru Kaskazini.

Masao alisema suala la majanga halina hodi, hivyo ni vyema jamii ikawa na mfuko maalumu wa kusaidiana linapotokea tatizo kama hilo.

Alisema kuwapo kwa mfuko maalumu ambao utakuwa na bima maalumu, utasaidia kutatua mzigo kwa serikali ya kumsaidia mwananchi mmoja mmoja.

"Ndani ya serikali kuna mfuko wa maafa, nipende kutoa ushauri kwa jamii kuanzisha mfuko huo utakaokua ukisaidia linapotokea tatizo kama la Deogratias...sisi wana ushirika tumeguswa na tatizo hili na ndiyo maana nashauri jamii iwe na utaratibu wa aina hiyo," alisema Masao.

Awali, akizungumza kwa niaba ya serikali, Mtendaji wa Kijiji cha Ongoma, Helena Kissae, amekiomba Chama cha Ushirika kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu katika kijiji hicho.

Alikishukuru chama hicho kupitia mradi wao wa muungano wa vyama vya ushirika kwa kutoa msaada wa mabati 20 kwa muathirika wa moto ambaye kwa muda wa mwezi amekua hana mahali pa kuishi yeye na familia yake.

Kwa upande wake muathirika aliyeunguliwa na nyumba yake na kupoteza fedha taslimu zaidi ya Sh. milioni 20 amekishukuru Chama cha Ushirika Uru Kaskazini, kupitia mradi wa pamoja kwa kumsaidia mabati 20.



Ukurasa 18

Anena mafanikio: Nilianza kimasihara kuku 12, leo wako 430



Ukurasa 16

Wanawake wa Geita wanavyojitosa kuchimba madini mgodi wa dhahabu


# BUFE

Ijumaa Mei 3, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## ILO inavyozungumzia ajira duniani

Ukurasa 15



# Aliyetegemea kuomba na vibarua shambani, leo ana miradi

**Na Elizabeth Zaya**

'PENYE nia pana njia', ni usemi wa Kiswahili. Katika uhalisia wake, ni tamko linalofaa kubebwa na Rose Samson (32), mkazi wa kijiji cha Mayale katika Halmashauri ya Makambako, mkoani Njombe, kulingana na hatua aliyofikia.

Ukimuona sasa, mara zote ni mama wa kuwajibika. Kila mara yuko barabarani na si ajabu akakutekeleza ghafla, akikimbia kwenda kuwasikia wateja wake. Madereva wa mabasi wamekuwa marafiki wake wakubwa kibiashara.

Nipashe ilishuhudia, mara nyingi kutoka nyumbani kwake jirani na barabarani, madereva wasipomkuta barabarani, wanampigia honi kumuita kwa ajili ya biashara au mahitaji mengine katika uhusiano wao wenye sura ya biashara, iliyobeba ishara ya kuaminika na kukubalika kwa mama huyo.

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

# Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

## MAKUU KUPITIA TASAF...

# Aliyetegemea kuomba na vi shambani, leo ana miradi ili

• Alijinasua kwa kuni, mayai, kuku, sasa... • Asomesha n akiota makuu • Siri ya mafanikio ni adha ya kutelekezv

**INATOKA UK.13**

Huyo ni mama wa watoto watatu, mwenye simulizi ya ndoa yake ilivyoingia utatanishi wa kukimbiwa na mumewe aliyemkimbia na kumtelekeza, huku akimwachia mzigo wa kulea watoto walioshi kwa tabu.

Anasema, wakati huo waliishi eneo la Igawa, katika wilaya ya Mbarali, ambako ni jirani na mpaka wa Mkoa wa Mbeya.

**SHIDA ILIKOANZIA**

Ni safari ya miaka miwili bila ya kuwa na mume na shida zilizokithiri, ndipo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ilipomuona katika dimbwi hilo la umasikini.

Rose anasema, wakati anaolewa na mume wake anayemtaja kuwa mtaalamu wa misitu wa serikali, kwa muda wa miaka saba waliishi vizuri sana, kabla ya mume huyo kubadilika ghafla, hata kufikia kutoweka nyumbani.

"Tabia ya mume wangu ilianza kubadilika sana, akawa siku moja moja harudi nyumbani, anarudi kesho yake, lakini baadaye tabia hiyo ilizidi mpaka ilipofikia akaondoka kabisa nyumbani, alikimbilia Dar es Salaam na mwanamke mwingine," anasimulia Rose na kuongeza:

"Hapa nyumbani aliniacha na watoto tukiwa hatuna hata chakula cha kututosha na nilikuwa namuuguza mama yangu mzazi ambaye alikuwa anaugua kwa kipindi kirefu (baadaye alifariki).

"Nyumba tuliyokuwa tunaishi ilikuwa ni ya nyasi na ilipokuwa ikifika katika kipindi cha masika, ilikuwa inadodosha maji ndani hata kama tumelala."

Rose anasema, kadri siku zilivyosogea, ndivyo maisha yalivyozidi kuwa magumu na kwamba kila alipojaribu kuwasiliana na mume wake kumuomba msaada, hakuwa tayari kumsaidia.

"Nilikuwa navumilia 'najitosa' kumpigia mume wangu simu kumuomba msaada nilipokuwa



Rose Samson akihudumia kuku wake na mayai nyumbani kwake Makambako. **PICHA ZOTE: ELIZA ZAYA.**

> **"Tabia ya mume wangu ilianza kubadilika sana, akawa siku moja moja harudi nyumbani...**

naona hali imezidi kuwa ngumu, lakini alizidi kunipa majibu mabaya na akikataa kunisaidia.

"Baadaye, sijui aliona kama namsumbua alibadilisha namba ya simu, kwa sababu simu yake ilikuwa haipatikani tena," anasimulia Rose.

**VIBARUA HADI TASAF**

Rose anasema, baada ya hali kuwa ngumu zaidi, alitafuta vibarua vya kufanya, kujipatia walau fedha za chakula na kujikimu kimaisha kwa jumla.

"Nilianza kufanya vibarua vya kukata nyasi, kuvuna mahindi, riziki yoyote niliyokuwa napata katika kazi hizo, ndiyo nikawa natumia kununua chakula nakula na watoto,"anasema Rose.

Anasema aliishi kwa vibarua zaidi ya miaka miwili, ndipo alipoingizwa katika mpango wa TASAF wa Uhawilishaji Fedha wa Kunusuru Kaya Masikini.

"Wakati TASAF wanakuja, kwa kweli nilikuwa 'nimechoka' mno. Nakumbuka nilichaguliwa katika mkutano wa kijiji, mkutano ambao ulikuwa unaangalia kaya zilizo masikini katika kijiji kwa ajili ya kuingizwa katika mpango wa kusaidiwa, ndipo na mimi nilichaguliwa," anasimulia.

Rose anaendelea: "Kwa kweli siku ile niliiona kama ilikuwa ya muujiza kwangu, baada ya wa-



BIASHARA
ILO inavyozungumzia ajira duniani
Ukurasa 15

UCHUMI
Wanawake wa Geita wanavyojitosa kuchimba madini mgodi wa dhahabu
Ukurasa 18

BIASHARA
Anena mafanikio: Nilianza kimasihara kuku 12, leo wako 430 wanaoniajiri
Ukurasa 19

# ibarua yoajiri

mtoto 'academy'
wa



nakijiji kunichagua. Tasaf walikuja nyumbani kwangu kuangalia mazingira yangu, wakanihoji maswali na mimi nikajieleza. Kwa hiyo wakaniunga katika mpango na nikawa napewa Sh. 44000,"

"Wakati nimechukua awamu ya kwanza, mama yangu alikuwa bado anaumwa. Nikachukua ile hela awamu ya kwanza, nikampeleka hospitali.

**ALIVYOIBUA MTAJI**

"Wakati pesa ya awamu ya pili, inaletwa nilikuwa nimeomba nifanye kibarua cha kusafisha shamba. Nikawa nimemuomba mwenye shamba asinilipe pesa, isipokuwa aniachie kuni zilizopo shambani, ndiyo ziwe malipo yangu, ambaye kweli alikubali na kuniachia.

"Nilipata lori nne za kuni na nikatumia Sh. 44000 niliyopewa na Tasaf. Awamu ya pili nikakodi gari kwa ajili ya kunibebea kuni, hizo kwenda kuuza na kulipa watu walionisaidia kupakia.

"Kweli Mungu ni wa ajabu. Nilifanikiwa kuuza roli tatu kwa shilimgi 190,000 na kuni nyingine ikakosa mteja, nikawa natumia nyumbani," anasimulia namna alivyoanza kufanikiwa.

Rose anasema, baada ya kupata kiasi hicho cha fedha kwenye kuni, aliongezea Sh.44000 ya Tasaf ya awamu ya tatu, ikafika Sh. 230, 000, akanunua mayai na kuanza kuyauza barabarani kwa abiria na watu wengineo.

Anasema, aliendelea na biashara hiyo ya mayai barabarani, huku akitumia fedha anazopatiwa na Tasaf kwa ajili ya watoto shuleni na chakula.

**AHAMIA UFUGAJI KUKU**

"Nilivyoona biashara inatoka nikaendelea, nikiona imetoka zaidi naongeza mtaji. Tasaf walivyokuja kunifanyia tathmini tena wakaniongezea mtaji wa kuku. Nikakazana zaidi kufanya kazi zangu, wakati naendelea kufuga huku nauza mayai,"anasimulia Rose.

"Mwaka 2017 ndiyo ulikuwa mwaka wangu wa kwanza kuuza kuku wakiwa 200, nilipata hela ambayo niliongezea na ya mayai nikaanza kujenga nyumba, nilibakisha kuku sita tu, wakike wanne na wa kiume wawili ili waendelee kuzaa," anasimulia

Anasema kwamba, aliendelea na biashara hizo za kufuga na kuuza mayai na kwamba mwaka 2018, alifanikiwa kupandisha nyumba yake na kuezeka.

"Kuku wangu mimi huwa navuna (kuuza) mwisho wa mwaka. Huwa siuzi kabla ya hapo kwa sababu huwa nasubiri wawe wengi ili nikiuza, pesa ninayopata nifanyie kitu cha maana. Kwa hiyo, katika kipindi hiki ambacho naendelea kufuga huwa nategemea biashara ya mayai," anasema Rose.

Rose anasema, katika biashara ya mayai, mpaka sasa amejitanua na anaweza kuuza kati ya trei sita hadi tisa kwa siku na kwamba ana wateja wengi ambao wamekuwa wakinunua kwake na kupeleka mjini kwenda kuuza.

Mbali na biashara hizo, Rose anasema anaendelea kujitanua kuongeza biashara nyingine, mojawapo ni shamba, kwani awali hakuwahi kuwa nalo, lakini kupitia

msaada wa Tasaf na biashara zake, amenunua shamba ekari tatu.

Anasema, kwa sasa analima mahindi na maharage na kutokana na kuendesha biashara ya ufugaji kuku na kuuza mayai, amewakodisha watu fedha za kumsaidia kusafisha, kulima na kuvuna mazao yake, ikiwa ni ishara tosha ya ushindi, kuliganisha na alikotoka.

**INATOKA UK.20**

# ILO inavyozungumzia ajira duniani



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Guy Ryder. **PICHA: MTANDAO**

**Na Padre Richard A. Mjigwa,** Vatican

JUZI ilikuwa Siku ya Wafanyakazi Duniani, maarufu Mei Mosi. Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Guy Ryder, anasema maadhimisho ya Jubilei ya Miaka 100, ni fursa kwa shirika lao kutathmini mustakabali wake.

Anasema, hiyo inatokana na ukweli kwamba, mazingira ya kazi yanapitia mabadiliko makubwa, kiasi cha kuibua hisia za hofu na shaka kwa sasa na siku zijazo.

Hiyo inaendana na changamoto kubwa, kutokana na mapinduzi ya makubwa ya sayansi na teknolojia yanayotishia fursa za ajira kwa mamilioni ya watu duniani.

Katika maadhimisho hayo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, anahimiza umuhimu wa sekta ya kazi duniani kujikita katika ubunifu, ili kuimarisha uchumi na kupiga hatua katika malengo endelevu na fungamani ya binadamu.

Mabadiliko katika mfumo wa kazi, uhusiano na kufungamana katika maeneo hayo na umuhimu wa mapumziko kwa wafanyakazi, ni mambo yanayopaswa kuzingatiwa, ili kuongeza tija na ufanisi kazini.

Anataja mabadiliko makubwa yanayojitokeza kazini, ni tishio kwa wafanyakazi duniani na kuna haja kwa jumuiya za kimataifa, kuwekeza zaidi katika sekta ya elimu, itakayowaandaa vijana wa kizazi kipya, kukabiliana na changamoto za fursa za kazi na ajira kwa sasa na baadaye.

Guterres, anasema sera na mikakati ya kiuchumi ni muhimu kuwahakikishia usalama, ustawi na maisha bora wailioko hatarini kuathirika kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia kazini.

Ni changamoto anayoitaja inapaswa kuvaliwa njuga na serikali na wadau wake katika sekta za uchumi, uzalishaji na huduma.

Anasema, dunia inaendelea kujiimarisha katika mfumo wa kidigitali, hali inayotishia kwa kiasi kikubwa fursa za ajira kwa wengi.

Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Maria Fernanda Espinosa, anakumbusha zaidi ya watu milioni 40 wameathiriwa na mifumo ya utumwa mamboleo na kwamba watu milioni 190 hawana ajira, theluthi tatu ni vijana.

Anasema, katika muktadha huo, jumuiya ya Kimataifa inapaswa kuhakikisha inafikia lengo Namba nane la Malengo ya Maendeleo Endelevu, kutoa ajira bora zaidi, ili kupambana na umaskini duniani sanjari na ukosefu wa haki.

**BEI YA MAZAO >>** MCHELE 184375/- | ULEZI 142642.9/- **FEDHA >>** RAND 164.66 | KSH 22.75 | USH 0.61

BIASHARA

# Wanawake wa Geita wanavyojitosa kuchimba madini mgodi wa dhahabu

• Walia bado'50 kwa 50' kazini haijatimia • Waneemesha serikali huduma mamilioni

**Na Shaban Njia,** Geita

MIAKA ya nyuma, mwanamke alichukuliwa kwenye jamii kuwa ni mama wa nyumbani na hawezi kufanya kazi zinazoweza kufanywa na mwanaume. Kazi yake kubwa ilibaki kupika na kulea watoto, akiaminika hawezi kufanya kingine chochote na jamii haikumpa nafasi.

Hivi sasa kuna mageuzi, kuna wanawake wanaomiliki mashamba, maduka na wengine wana viwanda vidogo na vikubwa.

Katika mikoa ya Geita na Shinyanga, wanajihusisha na biashara zinazowasaidia kujijenga na kujiinua kiuchumi, hasa maeneo ya machimbo madogo ya dhahabu na kuzisaidia familia zao kusoma bila ya kuwategemea waume zao.

Maeneo hayo yameibuka kuwa sehemu mbadala ya kujipatia kipato hicho. Kuna makundi makubwa ya wanawake wameingia katika kujishughulisha na kazi hizo; kuchimba madini, pia kununua madini na kuuza.



Flora Kishepo, akiosha mchanga wa dhahabu kwa kutumia karai ndogo, inayoumika kutambua wingi wa madini ya dhahabu kwenye udongo katika mgodi mdogo wa Nyakafulu, mkoa wa Geita.

### WACHIMBAJI WASIMULIA

Regina Paskali (40), ni mzazi wa watoto saba na mkazi wa kijiji na kata ya Nyakafulu, katika Halmashauri ya Mbogwe wilayani mkoani Geita, anasema uchimbaji madini walioanza rasmi mwaka 2006, umebadili maisha yake kwa kiasi kikubwa, tofauti na ilivyokuwa awali.

Anaeleza, tangu alipoanza uchimbaji madini mpaka sasa ana miaka 14, amekuwa akinufaika na shughuli hiyo, hata kufikia hatua ya kuchangia maendeleo ya kata katika Afya, Elimu na Maji, huku akihudumia familia pasipo vikwazo vikubwa kimaisha.

Mama huyo anasema, licha ya kufafanikiwa sawa na kinababa katika kazi hiyo, anataja changamoto iliyopo ni ugumu wa kazi, akilalamika kuugua kiuno kila mara wakati wa uoshaji mchanga.

Flora Kishepo, anajihusisha na ununuzi wa mawe ya dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo, ikiwamo mchanga wa madini, anayasaga na kuosha akitafuta madini ndani yake.

Anasema, aliamua kuingia katika uchumi huo, baada ya kuona wanawake wenzake waliotelekezwa na waume, wamefanikiwa kimaisha na kunufaika.

### KABLA UCHIMBAJI

Regina anasema, kuwa kabla

> **"Aliamua kuingia katika uchumi huo, baada ya kuona wanawake wenzake waliotelekezwa na waume, wamefanikiwa kimaisha na kunufaika.**

ya uchimbaji kuanza katika Kata ya Nyakafulu, kinamama wengi walijishughulisha na kilimo, pia wakilea watoto majumbani.

Analaumu hilo kuwa ni jambo lililowafanya wabweteke na maisha ya utegemezi kwa waume zao, huku uchumi wao ukiwa katika hali mbaya, lakini hatua waliyochukua sasa, maisha yamebadilika kwa kiwango kikubwa.

### VIFAA KAZI BORA

Regina anasema katika mageuzi hayo, wamepata zana za kisasa kuchimbia madini, ambayo katika eneo la Nyakafulu yanaonekana kuwa mengi na kuweza kuwaongeza kipato, pia serikali kufaidika kwa tozo na kodi mbalimbali.

Anasema, wamekuwa wakitumia vifaa vya kizamani vilivyowafanya kutumia nguvu kubwa



Regina Paschali, akiwa kazini. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

wakati wa uchimbaji na uchenjuaji madini, huku madini mengi yanabaki kwenye mchanga ambao wanawauzia wenye viwanda kuufanyia kazi.

Anasema, wameshaiomba serikali kuwawezesha vifaa vya kisasa vya uchimbaji kwa ajili ya kuendesha shughuli hiyo, kwani nao wana uwezo wa kushiriki katika uchimbaji wa madini, sawa na wanaume.

### MASOKO JE?

Regina anasema, baada ya serikali kuanzisha soko la kisasa la wachimbaji wadogo mkoani Geita, anakiri kuwa ni neema, kwani awali madalali walinufaika kwa kiasi kikubwa.

Sambamba na soko, anataja kuondolewa baadhi ya tozo iliyokuwa moja ya changamoto kwao wachimbaji, kiasi cha baadhi yao wakiwemo kinamama, walidhulumiwa madini na madalali, sasa mazingira mapya yameweka mambo shwari zaidi.

### UCHANGIAJI MAENDELEO

Regina anasema, uchangiaji maendeleo katika kata ya Nyakafulu, kupitia Ushirika wa Isanjabadugu yalipo machimbo, umesaidia mengi ya kimaendeleo, kwa miaka miwili ya kuwapo kwake, mfano hai katika tajwa za Maji, Elimu, Miundombinu na Afya.

Mastula Samwel, ni Makamu Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo katika Mgodi wa Nyakafulu Isanjabadugu, anasema wao ni vinara wa uchangiaji, kuliko mkoa mzima wa Geita.

Anasema, kupitia wachimbaji hao wamejenga nyumba za walimu, ofisi ya mtendaji, pamoja na mambo mengine mbalimbali na kwa ujumla mkoa huo, hususani Wilaya ya Mbogwe, ndio mgodi huo ulipo.

Samweli anasema, mgodi huo tayari umeshalipa mapato ya serikali kwa kipindi cha miaka miwili tangu uanzishwe, Sh. milioni 300 na kuongoza katika ulipaji kuliko migodi yote midogo mkoani Geita.

Anasema, katika miundombinu ya barabara, wachimbaji hao wa Nyakafulu Isanjabadugu, wametumia Sh. milioni 28 kuchangia ujenzi wa barabara yao kiwango cha Changarawe, yenye umbali wa kilomita mbili, wakitumia Sh. milioni 86.9 katika kipindi hicho.

Pia, Samweli anasema, ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, wamelipa mrabaha wa Sh. milioni 336, huku ushuru wa huduma ni Sh. milioni 66.

Katika fedha hizo, Sh. milioni 18 walilipa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, huku kijiji cha Nyakafulu kikipata Sh. milioni tatu.

Makamu Mwenyekiti huyo, anasema wanatarajia kujenga madarasa manne yenye thamani ya Sh. milioni 44, kituo cha afya chenye thamani ya Sh.milioni 76 na tayari wamefanikiwa kwa asilimia 75 kwa kipindi cha miaka mitatu.

Katibu wa Mgodi wa Nyakafulu Isanjabadugu, Stephen Moses, anasema wao wachimbaji wadogo wamejitahidi kutunza mazingira kwa kiwango kikubwa na kuwa katika orodha ya migodi safi katika ukanda huu wa Ziwa Victoria.

### AJIRA ZA WATOTO

Moses anasema, katika mgodi huo tayari wameweka matangazo ya kukataza ajira za watoto, kuanzia uchotaji maji, uchenjuaji na uchimbaji.

Pia, anasema wachimbaji wamefanikiwa kuwazuia wenzao kuja katika miradi na familia zao, hata kuendesha shughuli za kilimo, lengo ni kuwahakikishia wanakuwa salama. Wanatumia Kituo cha Polisi Mbogwe, kuwasaidia.

Moses anaendelea kusema, kuna jumla ya wachimbaji 2000 wanaopatikana mgodini, wengine wanafanya biashara ya umachinga, mamalishe, kuchota maji na jumla yao kuna watu 5,000.

### MIKOPO YA MADINI

Regina anajigamba, uchimbaji unaofanywa na wanawake sio wa kisasa, ukilinganishwa na wanaume, lakini bado umekuwa wa manufaa makubwa kwao, kama kuwapeleka watoto shule.

Anasema, mbali na mikopo katika taasisi za kifedha na halmashauri kuinua mitaji yao na kununua dhahabu, imewabadilisha haraka kimaisha, kufikia haki ya kukopeshwa.

Pia Flora, anazungumzia changamoto kwamba, wamekuwa wakidharauliwa na wanaume kwamba hawawezi kazi ya uchimbaji madini, pia wanadhulumiwa mchanga wa madini.

Pia, anataja wingi wa maji mashimoni, inawaingiza gharama kubwa wakati wa kuyaondoa, kutokana na maeneo hayo kukosa huduma ya nishati ya umeme, wanakolazimika kutumia genereta.

Flora anatoa rai kwa kinamama wasiogope kufanya kazi zinazofanywa na wanaume, bali wajitume kuuchimba madini ya dhahabu.

# Biashara katika picha



Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Atashasta Nditiye, akimsikiliza Meneja Mauzo wa kampuni ya Simu ya Airtel, Baraka Ndelele, wakati alipotembelea banda hilo katika maonesho ya Wiki ya Maadhimisho ya Miaka 10 ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), yaliyofanyika, jijini Dodoma. **PICHA: AIRTEL**



Machinga akiwasiliana kwa simu wakati akisaka wateja wa bidhaa zake, katika eneo la Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Mfanyabiashara ndogondogo akihama na meza yake kutafuta eneo la biashara Ubungo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52625/-| MAHARAGE 170000/-

BIASHARA

MUUZA MAJI 'MSTAAFU'

# Anena mafanikio: Nilianza kimasihara kuku 12, leo wako 430 wanaoniajri

• Ndoto yake wafike 23,000 'atoke' kimaisha



Mmoja wa vijana wanaomsaidia Jesca kazi ya ufugaji, Edson Haule, akiwapa kuku chakula.

**Na Sabato Kasika**

DHANA ya ujasiriamali ina maana pana na kwa kawaida, mjasiriamali ni mtu mwenye hamasa ya kuleta mabadiliko chanya, katika hali yake ya kiuchumi na maendeleo. Hiyo ni kwa maana ya kujiajiri na hali nzuri zaidi kiuchumi.

Kwa kifupi, mjasiriamali anaweza kuwa mtu yoyote, aliyejiajiri katika sekta au shughuli fulani, kama vile ufugaji, kilimo au biashara halali.

Ujasiriamali kwa sasa, una nafasi kubwa nchini, kwani baadhi ya watu wamejiajiri kutokana na juhudi za serikali kuboresha sera na sheria mbalimbali za uchumi, ikiwamo ya maendeleo ya biashara ndogo.

Kutokana na juhudi hizo za serikali, baadhi ya Watanzania sasa wanajitoa kimasomaso kuanzisha biashara au kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali, kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

Jesca Ndaro, ni miongoni mwa kada hiyo ya Watanzania, aliyejikita katika ya biashara ya kufuga kuku wa kienyeji na chotara nyumbani kwake, eneo la Mbezi Mshikamano, jijini Dar es Salaam.

> **"Ukweli ni kwamba, kuku wa kienyeji huchukua muda mrefu na uzalishaji wake ni mdogo, lakini bado wana soko kubwa, ndio maana sitegemei hao.**

Mjasiriamali huyo alizungumza na Nipasahe, akiwa na maelezo marefu kuelezea yenye smulizi ya alivyoanza biashara hiyo, mafanikio, changamoto, malengo ya baadaye, katika kuboresha ujasiriamali huo. Ifuatayo ni mazunguzo ya maswali na majibu:

**SWALI: Kwa nini na lini uliamua kuanzisha biashara ya kuku? Ulikuwa na mtaji wa Sh.ngapi, idadi ya kuku wangapi na sasa wamefika wangapi na sasa una mtaji wa Sh. ngapi?**

**JIBU:** Nilianza tangu mwaka 2004. Nilikuwa nikifuga kuku wa kienyeji wasiozidi 12, kwa ajili ya matumizi ya kifamilia, lakini Februari 2010 ndipo nilipoanza rasmi kuongeza kuku wa kienyeji wa kufuga kwa ajili ya biashara, wakiwa 36.

Niliongeza kuku kwa sababu ya soko kubwa lililopo, pia mapenzi yangu juu ya hawa kuku wa kienyeji. Mtaji niliyoanza nao ulikuwa Sh. 180,000. Wakati huo, hawa kuku walikuwa wakilala chumba kimoja cha nyumba yangu, asubuhi nawaachia nawapa chakula kidogo.



Mjasiriamali Jesca Ndaro. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA.**

Baadaye mwaka 2012, waliongezeka na kufikia kuku 96, nikajenga banda dogo nje ya nyumba yangu. Mwaka 2013 niliibiwa kuku 24, hivyo nikawa nimepata changamoto kubwa kwa kurudi nyuma.

Niliendelea kufuga kuku waliobaki, hata hivyo magonjwa ya kuku kama 'kideri' yaliniathiri na kuua kuku wengi, hivyo nikabakiwa na kuku 26 tu.

Mwanzoni mwa mwaka 2014 nilikutana na mtotoleshaji wa vifaranga maeneo ya Zone huku Mbezi Luis, nikanunua vifaranga 50 wa kienyeji. Hata hivyo, vifaranga wengine walikufa, wakabaki 27.

Baadaye September 2014, nilianza kununua vifaranga 100 aina ya chotara na wakati huo nikiwa na kuku wa kienyeji kama 42 tu. Baada ya kununua chotara.

Changamoto iliyokuwepo ni magonjwa ya kuku, japo vifaranga kama 69 walifanikiwa kukua hadi kuanza kutaga mayai. Aprili mwaka 2015, niliboresha na kujenga banda jipya kwenye eneo langu lenye uwezo wa kuchukua kuku 180.

Hadi kufikia Novemba mwaka huo, nilikuwa na kuku 122 tu. Baada ya hapo, Januari 2016, nilinunua vifaranga 200 na kuongeza banda lingine linalobeba kuku 150, hivyo nikaongeza na kupanua biashara hii.

Sasa nina kuku 430, wakiwamo 112 aina ya chotara na wa kienyeji, pia nimefanikiwa kununua incubator ( mashine ya kutotolea) ndogo ya kuweka mayai 180. Jumla ya mtaji wangu sasa hivi ni kama Sh.milioni nne.

**SWALI: Naona safari ya biashara yako ni yenye mafanikio, nini siri ya ushindi huu?**

**JIBU:** Nilipenda sana ufugaji wa kuku baada ya kukutana na mmiliki wa (shamba la mifugo) Msigani Poultry Farm, ambaye alinielezea historia yake.

Pia ufugaji wa kuku unahitaji kujituma na uvumilivu na mwisho msaada wa wataalamu. Nimekuwa namtumia daktari wa mifugo, ambaye ndiye mshauri wangu anayenitembelea mara kwa mara.

**SWALI: Soko lako ni lipi? Biashara ya kuuza kuku mmoja mmoja au jumla?**

**JIBU:** Soko la biashara yangu, ambayo ni kuku na mayai, ninauzia kwa mteja mmoja mmoja, wale wanaonunua jumla, hasa kwa wenye sherehe. Pia, wanunuzi wanaotoka kwenye masoko ya Manzese, Magomeni, Kisutu na Buguruni.

Ukweli ni kwamba, kuku wa kienyeji huchukua muda mrefu na uzalishaji wake ni mdogo, lakini bado wana soko kubwa, ndio maana sitegemei hao.

Hivi sasa wapo wa kienyeji

FEDHA >> USD 2,300.96| Pauni 3,011.73| Euro 2,595.25

# Anena mafanikio: Nilianza kimasihara kuku 12, leo wako 430 wanaoniajri

wanaendelea kukua, pia hapo baadaye ninategemea kuongeza matabaka zaidi ya kuku. Kama nilivyosema awali, mwanzoni nilifuga kuku wa kienyeji, lakini kulingana na mahitaji ya soko, nilianza kufuga chotara.

Hata hivyo, bidhaa zangu kuku wa kienyeji kama mayai bei yake iko juu na hawapatikani sana, hivyo mahitaji yapo na hata kuku wa kienyeji huuzwa kwa bei kubwa, ukilinganisha na kuku wengine.

**SWALI: Unafanya biashara hii pekee yako au kuna watu wengine unasaidiana nao, kama wapo mgawanyiko wa kazi kutwa nzima na wenzako ukoje?**

**JIBU:** Katika biashara hii nimeajiri vijana wawili wa kiume, mmoja anashughulika na kuku wa kienyeji na mwingine chotara.

Kwenye suala la ubia, ni kwamba sijafikiria kwenda huko, labda, huko baadaye. Hata hivyo, hivi sasa niko katika kusajili jina la biashara pale Brela. Pia, huwa ninapata ushauri wa mtaalamu aitwaye Lenox Kayanda.

**SWALI: Hatua uliofikia umeridhika nayo au unataka kwenda mbele zaidi? Mkakati wako kiutendaji ukoje?**

**JIBU:** Hatua niliyofikia sijaridhika bado. Ninataka kwenda mbele zaidi, Nimenunua ekari mbili na nusu eneo la Kongowe Kibaha na nimeanza kujenga mabanda mawili ya kuku. Huko Morogoro ninalo shamba la ekari mbili hivi, liko jirani na kituo cha treni ya mwendokasi inayojengwa.

Pia, ninajua baadaye nitapata nafuu kusafirisha mazao kuja Dar es Salaam na ninatafuta eneo Dodoma, ambako nimeona fursa ya mahitaji ya bidhaa za mifugo kama mayai na kuku wa kienyeji.

Vilevile maono yangu ya mbele, ni kuzalisha vifaranga, kupanua mradi nifikie kuku wa kienyeji 3,000 na wengine ambao ni chotara 20,000.

Siyo kwamba ninataka kuishia kiasi hicho tu, bali nikifikisha kuku 23,000 nitajiona kama na mimi ni mfanyabiashara mkubwa.

Ninaamini kiasi hicho kinanitosha kukihudumia, kabla ya kuongeza idadi nyingine, hasa kwa kuzingatia kwamba kuku wa kienyeji kuwatunza kuna gharama hawana soko kubwa, lakini chotara wana soko sana kwenye mayai.

Hivyo, nikiwa na 20,000 ninaweza kupata mayai na kuyauza pia kwa wingi, kwani watu wanaohitaji mayai ni wengi. Lakini, kadri biashara itakapochanganya, ninaweza kuwa na wengi zaidi.

**SWALI: Shughuli yoyote haikosi changamoto. Kwako hili likoje. Je, unaweza kuniambia hali halisi ya changamoto unazokabiliana nazo katika maeneo mbalimbali kwa ujumla wake?**


Jesca akihudumia kuku wake nje ya banda.

**JIBU:** Changamoto zipo. Kwanza, magonjwa ya kuku huathiri sana biashara hii, kama nilivyojibu swali la kwanza.

Ila nategemea mtaalamu wa mifugo anayenishauri, amnaitwa Lenox Kayanda, huwa ananitembelea mara kwa mara kuangalia uzalishaji wangu na kunishauri juu ya magonjwa kama kideri, 'typhoid' (homa ya matumbo) ya kuku na mengine.

Changamoto ya pili, ni uhakika wa upatikanaji vyakula bora vya kuku na gharama kuongezeka kila mwaka na changamoto ya tatu, ni mabadiliko ya bei za mazao ya kuku, kama mayai kwani zinashuka na kupanda wakati chakula bei zikipanda huwa hazishuki.

**SWALI: Kwenye biashara yako ni maeneo yepi yanayokugharimu kipesa kuhudumia kuku, uendeshaji biashara na gharama kisheria kama vile kodi, leseni na mambo mengine muhimu?**

**JIBU:** Gharama kubwa ziko kwenye chakula, ila kwenye mifugo hakuna kodi wala leseni. Hivyo, ninaishukuru sana serikali katika hilo.

**SWALI: Kutokana na sura ya mafanikio yako katika biashara, kuna watu wanaovutiwa kutoka kwako?**

**JIBU:** Ni kweli wanaovutiwa kutoka kwangu wapo wanaokuja kujifunza. Nami, huwa ninawahamasisha ili wafanye biashara kama hii wakitambua kuwa ina changamoto.

Lakini, siri kubwa ni kutokata tamaa, kwani hakuna biashara yoyote ambayo mtu anaweza kuifanya akafanikiwa bila kukumbana na vikwazo njiani.

**SWALI: Kihistoria, kabla ya kuanza biashara ya kuku, ulikuwa unafanya shughuli gani zilizokuwezesha uishi kiuchumi?**

**JIBU:** Nilikuwa ninafanya biashara ya kuuza maziwa ya mtindi, fresh (maziwa ya kawaida), maji na juisi kwenye kioski, maeneo ya Kimara Stop Over (Dar es Salaam).

**SWALI: Nini wito wako wa jumla kuhusu shughuli zako na picha nzima ya biashara hiyo?**

**JIBU:** Wito wangu kwa ujumla, ninaomba serikali kupitia wataalamu wake, uzoefu miongozo rahisi kwa ajili ya sekta ya mifugo na iwe inayoanza mafunzo kila baada ya muda fulani kwetu sisi.

Pia, biashara hii ina tija sana. Hivyo, nina uhakika iwapo serikali itaboresha huduma za ugani, vijana wanaweza kujiajiri, hata wanaomaliza vyuo vikuu masoko yapo.

Cha msingi ni mbinu sahihi za kufuga ikiwemo kupunguza gharama, ili wapate faida.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Aprili 18, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Geita | Morogoro | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Lindi | Manyara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 57000 | 70000 | 53000 | 57000 | 48000 | 60000 | 40000 | 45000 | 80000 | 60000 |
| Mchele | 200000 | 210000 | 195000 | 130000 | 165000 | 185000 | 180000 | 160000 | 200000 | 200000 |
| Mtama | 40000 | 60000 | 35000 | 180000 | 71000 | 100000 | 80000 | 100000 | 150000 | 42000 |
| Uwele | 40000 | 60000 | 34000 | 180000 | 71000 | 110000 | NA | 100000 | NA | 100000 |
| Ulezi | 72000 | 140000 | 75000 | NA | 155000 | 150000 | 180000 | 150000 | 200000 | 120000 |
| Ngano | 87000 | 130000 | 160000 | 180000 | 163000 | NA | 98000 | 150000 | NA | 120000 |
| Maharage | 150000 | 220000 | 170000 | 170000 | 185000 | 150000 | 180000 | 140000 | 200000 | 130000 |
| Viazi Mviringo | 70000 | 80000 | 66000 | 70000 | 82000 | 75000 | 50000 | 90000 | 100000 | 60000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia April 3, 2019

| | Dsm | Arusha | Kibaha | Dodoma | Geita | Iringa | Bukoba | Mpanda | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petrol | 2,147 | 2,192 | 2,151 | 2,206 | 2,312 | 2,211 | 2,363 | 2,355 | 2,378 | 2,181 |
| Diseli | 2,192 | 2,196 | 2,196 | 2,250 | 2,357 | 2,256 | 2,407 | 2,400 | 2,423 | 2,186 |
| M'taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Aprili 23, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,482.82 | -0.18 |
| DSEI | 2,020.08 | -12.15 |
| Thamani za Hisa (bln) | 19,471.20 | |
| Mauzo | 16,751,775.00 | |
| Hisa | 47,125 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| ACA | 4,640 | -6.26% |
| KA | 110 | -4.35% |
| EABL | 4,840 | +0.83% |
| JHL | 9,250 | +1.09% |
| DSE | 1,280 | +98.46% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,578.38 | 2,605.09 |
| USD | 2,278.12 | 2,300.91 |
| KES | 22.57 | 22.75 |
| GBP | 2,986.62 | 3,017.64 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Aprili 23, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 4,640.00 | 4,950.00 | -6.26 |
| CRDB | 125 | 125.00 | 0 |
| DCB | 340 | 340 | 0 |
| DSE | 1,280 | 1,300 | -1.54 |
| EABL | 4,840.00 | 4,800.00 | 0.83 |
| JHL | 9,250.00 | 9,150.00 | 1.09 |
| KA | 110.00 | 115.00 | -4.35 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 1,020.00 | 1,020.00 | 0 |
| MBP | 490.00 | 490.00 | 0 |
| MCB | 500.00 | 500.00 | 0 |
| MKCB | 800.00 | 800.00 | 0 |
| MUCOB | 400.00 | 400.00 | 0 |
| NICO | 170.00 | 170.00 | 0 |
| NMB | 2,340.00 | 2,340.00 | 0 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| NMG | 1,500.00 | 1,400.00 | 0 |
| PAL | 400.00 | 400.00 | 0 |
| SWALA | 490.00 | 490.00 | 0 |
| SWIS | 1,700.00 | 1,700.00 | 0 |
| TBL | 10,000.00 | 10,000.00 | 0 |
| TCC | 17,000 | 17,000.00 | 0 |
| TCCL | 600.00 | 600.00 | 0 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 2,244.52 | 2,262.51 |
| UGANDA SHS | 57.47 | 61.52 |
| RWANDAN FRANC | 251.53 | 254.42 |
| BURUNDI FRANC | 218.12 | 219.77 |
| USD | 227,818.81 | 230,097.00 |
| POUND STG | 294,911.45 | 297,952.61 |
| EURO | 254,906.47 | 257,547.57 |
| CANADIAN $ | 169,470.22 | 171,114.00 |
| SWITZ. FRANC | 223,724.65 | 225,873.17 |
| JAPANESE YEN | 2,037.37 | 2,057.56 |
| SWEDISH KRONOR | 24,245.07 | 24,479.71 |
| NORWEG. KRONOR | 26,497.34 | 26,760.76 |
| DANISH KRONOR | 34,148.58 | 34,484.89 |
| AUSTRALIAN $ | 160,133.84 | 161,758.19 |
| INDIAN RPS | 3,258.88 | 3,290.44 |
| PAKISTAN RPS | 1,532.78 | 1,620.40 |
| ZAMBIAN KWACHA | 18,043.25 | 18,334.42 |
| MALAWIAN KWACHA | 289.17 | 309.43 |
| MOZAMBIQUE-MET | 3,537.56 | 3,567.40 |
| ZIMBABWE $ | 42.63 | 43.49 |
| SDR | 316,030.26 | 319,190.56 |
| GOLD (T/O) | 289,729,234.68 | 292,691,184.29 |
| S. AFRICAN RAND | 15,829.33 | 15,980.62 |
| UAE DIRHAM | 62,028.65 | 62,636.99 |
| SINGAPORE $ | 167,513.83 | 169,126.79 |
| HONK KONG $ | 29,049.63 | 29,338.63 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 60,751.68 | 61,354.29 |
| KUWAIT DINAR | 748,788.21 | 756,002.76 |
| BOTSWANA PULA | 21,141.59 | 21,537.08 |
| CHINESE YUAN | 33,906.65 | 34,229.93 |
| MALAYSIA RINGGIT | 55,228.80 | 55,713.56 |
| SOUTH KOREA WON | 197.63 | 199.26 |
| NEWZEALAND | 150,519.89 | 152,117.13 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **24/Apr/2019** | **2.30** | **2,307.00** | **2,298.50** | **2,300.97** |
| 23/Apr/2019 | 6.25 | 2,309.00 | 2,300.00 | 2,300.95 |
| 18/Apr/2019 | 11.55 | 2,308.00 | 2,292.00 | 2,300.90 |
| 17/Apr/2019 | 2.20 | 2,308.00 | 2,298.45 | 2,300.94 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **24/Apr/2019** | **70,700** | **5.75** | **5.00** | **5.17** |
| 23/Apr/2019 | 37,000 | 5.75 | 5.00 | 5.41 |
| 18/Apr/2019 | 43,000 | 6.00 | 5.00 | 5.45 |
| 17/Apr/2019 | 41,200 | 5.50 | 5.00 | 5.29 |
| 16/Apr/2019 | 53,550 | 5.50 | 4.90 | 5.24 |
| 15/Apr/2019 | 18,450 | 6.00 | 5.25 | 5.44 |

# Aliyetegemea kuomba na vibarua shambani, leo ana miradi iliyoajiri



Rose akihudumia kuku wake. **PICHA: ELIZA ZAYA**

"Kwa hiyo Tasaf wamenifanya niwe mwanamke jasiri na niko 'bize' wakati wote kuangalia shughuli zangu. Huwa sikubali kupoteza muda kabisa na kila siku akili yangu inazidi kupanuka kuona fursa ya biashara nyingine," anasema Rose.

**APANIA MAKUBWA**

Rose anasema lengo lake ni kutaka kuwa mnufaika wa Tasaf wa mfano, ili wenzake walioko katika kaya masikini wamuige na wajione wanaweza kupiga hatua kama watu wengine.

"Nilijifunza kuvumilia kwa kukipangia bajeti vizuri kile kidogo ninachosaidiwa na Tasaf na ndiyo maana nimefika hapa.

"Ninaomba na wenzangu wasikate tamaa bali wavumilie tu kwa kuendelea kutumia vizuri na kupangia vizuri bajeti hela anazopewa," anaeleza Rose.

Anataja mradi mpya aliyo nayo ni wa kufuga mbuzi, anaotarajia utamsaidia kumuongezea kipato zaidi.

"Yaani naweza kusema kwamba wamenitoa kwenye shimo. Hapa nilipo, nina mradi mwingine ambao walinigezea. Wamenipa mbuzi wawili wa kike na kiume," anasema Rose na kuongeza:

"Nimewafugia nyumbani kwa baba yangu na mpaka sasa wamefika nane. Niliwaondoa hapa nyumbani, kwa sababu watu sasa wameanza kunionea wivu,"

**AGEUKA MFANO**

Rose anasema hivi sasa amegeuka mfugaji wa mfano, anasema shughuli zake za ufugaji zimgeuka za mfano, hata kuwa sehemu ya mafunzo kwa vitendo kutoka chuo cha mifugo kilichoko jirani.

Kwa mujibu wa mjasiriamali huyo wa mifugo, ujio ya wanafunzi hao umwekuwa wa manufaa kwake kwani wamekuwa wakimasaidia moja kwa moja na kumuelimisha namna ya ufugaji bora, ambayo matokeo yake ni tija katika ufugaji wake.

Anataja mbinu mojawapo anayotumia ni kufuga mbwa aliyemfunza mengi hivyo kudhibiti wanyama waharibifu kuingilia mifugo wake.

Rose anasema, katika moja wa mafaniko aliyo nayo ni kwamba, anamsomesha mwanawe mmoja katika shule ya kisasa, ambako analipa ada ya Shilingi 700, 000 kwa mwaka katika mkoa wa Pwani.

**OFISA TASAF**

Mfuatiliaji wa Miradi ya Tasaf katika Halmashauri ya Makambako na Wanging`ombe, Edwin Mlowe, anasema lengo walilo nalo ni kuhakikisha wanapunguza umasikini katika kaya zenye changamoto za umasikini.

Anasema, hilo ndilo limewafanya, mbali na na kuwapatia fedha walengwa, wamekuwa wakijitahidi kubuni miradi mbalimbali ya kuwaanzishia, ili wajishughulishe katika hatua ya kuondokana na hali hiyo duni.

Akimzungumzia mafanikio ya wanachama wao Rose, anamsifu amekuwa mlengwa wa mfano, anayetumia vizuri mpango wa Tasaf katika kujiondolea umasikini na kuingia katika sura ya mafanikio kiuchumi.





# TUCTA yaguswa na miradi mikubwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi nchini (Tucta), limeipongeza Serikali kwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kwa maelezo kuwa inasaidia kuimarisha vyama vya wafanyakazi na kuongeza ajira kwa wananchi.

Akizungumza juzi katika maadhimisho ya siku ya Mei Mosi, Rais wa Tucta, Tumaini Nyamhokwa, alisema miradi hiyo inayotekelezwa pia inasaidia kuboresha maisha ya Watanzania.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa reli ya kisasa SGR), ufufuaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya na mradi wa umeme wa Stigler's Gorge.

Mingine ni upanuzi wa bandari mbalimbali, upanuzi wa viwanja vya ndege na utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo aliyosema inasaidia hata watoto wa maskini kupata fursa ya kusoma.

"Sisi tunaamini kuwa miradi hii inatusaidia kuimarisha vyama vyetu vya wafanyakazi maana inaajiri watu wengi ambao wanajiunga kwenye vyama vyetu vya wafanyakazi na kuongeza nguvu, lakini pia inasaidia kuboresha maisha ya Watanzania," alisema Nyamhokwa.

Aliishauri Serikali kuanzisha miradi mingine ikiwamo ujenzi wa viwanda vya kuchakata minofu ya samaki maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi kwa maelezo kuwa vitasaidia kuongeza thamani ya samaki hao. Vilevile alishauri Serikali kununua meli kubwa ya kubeba mizigo ili isaidie kusafirisha mizigo inayotoka nje ya nchi kwa kwa maelezo kuwa meli nyingi zinazosafirisha mizigo kutoka nje ya nchi.

Akisoma risala ya wafanyakazi, Katibu Mkuu wa Tucta, Yahaya Msigwa, aliiomba Serikali iwarejeshe watumishi wote wa darasa la saba waliokuwa wameajiriwa kwa kufuata sheria na taratibu zote za nchi lakini wakaondolewa.

Alisema baada ya serikali kuwaondoa kazini watumishi hao Tucta iliiomba serikali watumishi hao warejeshwe na baadhi walirejeshwa, lakini wamebaini baadhi ya wajiri hawakuwarejesha mpaka sasa na kwamba hata wachache waliorejeshwa hawajalipwa mishahara mpaka sasa.

"Vilevile tumebaini kuwa baadhi ya waajiri hawakuwarejesha watumishi hao na hata waliorejeshwa hawajalipwa mishahara yao mpaka sasa, tunaomba serikali itoe maelekezo kwa waajiri wote ili watekeleze utaratibu huo," alisema Msigwa.

Akijibu ushauri huo wa Tucta, Rais Magufuli alisema Serikali yake inaupokea na itaufanyia kazi na kwamba baadhi ya ushauri huo tayari ilishaanza kuufanyia kazi.

Alisema Serikali imeshaanza kujenga meli tatu katika Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria na baada ya hapo itaendelea na maeneo mengine.



Baadhi ya wanawake wa Kata ya Inyala, wilayani Mbeya, wakisaidiana kusuka nondo kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa Hospitali ya Wilaya hiyo, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bil. 1.5/- zaanza kujenga hospitali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SH. bilioni 1.5 zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbeya, zimeanza kutumika, baada ya wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri kuanza kujenga majengo saba ya awali.

Hospitali hiyo inajengwa katika Kata ya Inyala ambapo wananchi wamejitolea eneo kwa ajili ya mradi huo, huku wananchi hao wakijitolea nguvu zao kwa kubeba mawe, kuchota maji na kufyatua tofali.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema Kijiji cha Inyala kilijitolea eneo lenye ukubwa wa ekari 31 kwa ajili ya ujenzi bila kudai fidia, na kwamba wako tayari kujitolea eneo zaidi.

Alisema kata ina vijiji saba na kila Kijiji kimepewa kujenga jengo moja kutokana na mradi huo kujengwa kwa kutumia Accounti ya Dharura) kwa maelezo kuwa mfumo wa kutumia makandarasi unachelewesha miradi.

"Tunatarajia majengo haya saba yote yatakamilika Juni 30, mwaka huu na tumeamua haya majengo tuyajenge kwa haraka na kwa viwango ili serikali itupatie fedha zingine za kuendelea kujenga majengo mengine," alisema Kisemba. Aliyataja majengo yanayojengwa kwa awamu ya kwanza ni la wagonjwa wa nje (OPD), wazazi, kufulia, ghala la kuhifadhia dawa na jengo la upasuaji.

Mengine ni la Utawala, maabara ya la mama na mtoto, ambayo yote yanajengwa na mafundi wa kawaida wanaosimamiwa na Mhandisi wa Halmashauri.

Hata hivyo, Mwalingo alisema ujenzi wa hospitali hiyo umesaidia wananchi wengi wa Kata ya Inyala na maeneo jirani kupata ajira zikiwamo za kuuza vyakula na kusaidia mafundi.

Alisema mchango wa wananchi kwenye ujenzi wa hospitali hiyo unafikia thamani ya zaidi ya Sh. milioni 90 ikiwamo kusogeza mawe kwa ajili ya msingi na eneo walilojitolea.

Nao baadhi ya wananchi wa Kata hiyo, waliishukuru Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo kwa madai kuwa itawasaidia kusogeza huduma za matibabu jirani na makazi yao na kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu. Mmoja wa wananchi hao, Flora Mlowezi alisema hospitali hiyo itasaidia pia wananchi wa vijiji vya wilaya ya Mbarali ambavyo vipo jirani.

"Tulikuwa tunapata tabu sana kwenda kutibiwa jijini Mbeya ambako ni mbali, ilikuwa ikitokea mtu akazidiwa usiku tunaanza kuhangaika kumsafirisha hali ambayo ilikuwa inahatarisha maisha," alisema Flora.

Naye Felister Kaisi ambaye ni mkazi wa Kijiji hicho, alisema hivi sasa Wilaya ya Mbeya itakuwa na hospitali mbili kubwa ikiwa ni pamoja na Hospitali teule ya Ifisi zitakazosaidiana na vituo vya afya ambavyo vinaendelea kujengwa.

Kukamilika kwa hospitali hiyo kutasaidia wananchi wengi walio pembezoni na hiyo itakuwa hospitali ya pili kubwa katika Wilaya hiyo na hivyo kuboresha huduma za matibabu kwa wananchi.

## Wakunwa uchakataji wa dhahabu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

BAADHI ya wananchi wilayani Chunya, wameishukuru Serikali kwa kufungua viwanda vya kuchakata dhahabu vilivyokuwa vimefungwa kwa madai walikuwa wameanza kukosa ajira.

Hivi karibuni Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alifanya ziara ya kushtukiza kwenye viwanda vya kuchakata dhahabu wilayani humo na kubaini vikiwa vinakiuka sheria mbalimbali za madini ikiwamo kutorosha madini.

Baada ya kubaini hali hiyo, aliamua kuvifunga na kuwapa maelekezo ambayo walitakiwa kuyafuata ili avifungue na mwishoni mwa mwezi Aprili alitoa taarifa kuwa kati ya viwanda 38, 27 vimeshafunguliwa baada ya kutimiza masharti.

Baadhi ya wananchi waliishukuru Serikali kwa kuwafungulia viwanda hivyo wakidai kuwa walianza kupata wasiwasi ya maisha yao kuharibika.

Lawena Nsonda, mkazi wa Mji wa Makongolosi, alisema baada ya viwanda hivyo kufungwa watu wengi walikosa fedha, hivyo mzunguko wa fedha katika maeneo mengi ya wilaya hiyo ulipungua.


Alisema wafanyabiashara walikwama kutokana na kuwategemea watu wanaofanya kazi kwenye migodi na viwanda hivyo vya kuchakata madini kuwa ndio wateja wakuu wa biashara zao.

"Vyakula vilikuwa vinapikwa kwenye migahawa lakini vinaharibika kwa sababu wanunuzi walikuwa wamepungua, sasa hivi baada ya kuanza kufunguliwa biashara zimeanza kurejea katika hali yake ya awali, hivyo tunamshukuru Waziri," alisema Nsonda.

Aidan Mdimi, mmoja wa wamiliki wa migodi na viwanda vya kuchenjua dhahabu katika eneo la Kiwanja, alisema baada ya kufungiwa kiwanda chake ameingia hasara kubwa kutokana na kulazimika kuwahudumia wafanyakazi ambao walikuwa hawafanyi kazi yoyote.

Alisema ana wafanyakazi zaidi ya 100 wakiwamo madereva, wachimbaji na wanaofanya kazi kiwandani na baada ya kufungiwa kiwanda wote walibaki bila kazi yoyote, lakini walikuwa wanapata huduma kama kawaida.

"Nimeingia hasara kubwa sana, maana shughuli zangu zilikwama kwa zaidi ya wiki tatu, kuna baadhi ya magari niliyokuwa nimekodi na niliendelea kuyalipia pamoja na madereva wake... kwa sasa namshukuru Mungu nimesharekebisha kasoro zilizokuwapo na nimefunguliwa," alisema Mdimi.





# Ukosefu kituo cha afya wawatembeza kilomita 20

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WAKAZI wa Kijiji cha Msamalo, wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma ya kituo cha afya hali inayowalazimu kutembea umbali wa kilomita zaidi ya 20, kufuata matibabu.

Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, Edward Magulanga, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa kamati ya utekelezaji ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma (Uvccm) katika ziara ya kukagua shughuli za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya 2015 katika wilaya hiyo.

Alisema toka uhuru wakazi wa kijiji hicho hawajawahi kuwa na zahanati na kulazimika kutembea umbali huo kufuata huduma za matibabu katika vituo vya afya vilivyopo Chamwino Ikulu au Mvumi Mission.

Alisema wajawazito wengi wanajifungulia njiani, kutokana na changamoto mbalimbali.

"Wakati wa mvua za masika hali inakuwa ngumu zaidi kwa kuwa miundombinu ya barabara pia bado ni kikwazo wakati mvua zinanyesha, maji yanajaa katika makorongo hivyo huwezi kupita na kama una mgonjwa inabidi ajifungulie nyumbani bila kuwa na msaada wa kitabibu," alisema. Aidha alifafanua kuwa kutokana na hali, hivi sasa wameamua kunzisha ujenzi wa zahanati ya kijiji kupitia nguvu kazi za wananchi pamoja na mchango kutoka kwa mbunge wao. "Mbunge ametupatia mifuko ya saruji lakini pia wananchi wametoa nguvu zao katika kuchimba msingi na kusoma mawe"alisema.

Naye Mwenyekiti wa Uvccm Mkoa wa Dodoma, Billy Chidwabwa, aliwapongeza wananchi hao kwa kuanzisha ujenzi wa zahanati hiyo.

Alisema wao kama chama wanapongeza juhudi hizo za kuamua kuanza ujenzi wa Zahanati hiyo, kwani wanaunga juhudi za serikali katika kuboresha huduma za afya nchini.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kulia), akionyeshwa michoro ya mapangoni na askari wanyamapori, iliyochorwa zaidi ya miaka 1000, iliyopita na kabila la Wasandawe ambayo ni miongoni mwa vivutio vya utalii, wakati alipotembelea baada ya kuzungumza na watumishi wa Pori la Akiba la Swagaswaga katika ziara yake ya kikazi wilayani Chemba jijini Dodoma jana. Kulia ni Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mabula Misungwi. **PICHA: WMU**

# Takukuru yatakiwa kuingilia kesi za ukatili wa jinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI Mkoani Dodoma, imeitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kufanyia kazi malalamiko ya kesi za jinai, zitokanazo na ukatili wa kijinsia unaohusisha vitendo vya rushwa.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Chamwino mkoani hapa, Vumilia Nyamoga, wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau wa haki, jinai na utatuzi wa migogoro, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge.

"Takukuru fanyieni kazi jambo hili, rushwa za namna hii zisituharibie sifa ya mkoa wetu katika utoaji haki, kumekuwapo na malalamiko na tunazo taarifa kuhusu kesi kama hizi za jinai zinazotokana na ukatili wa kijinsia kuhusishwa na rushwa na hii imekuwa changamoto kubwa katika kushughulikia pale wanajamii wanapoamua kuelewana na kuyamaliza wenyewe huku wakiharibu ushahidi mahakamani," alisema Nyamoga.

Alisema pia kumekuwapo na malalamiko kuwa baadhi ya polisi kushiriki vitendo hivyo na kukwamisha juhudi za serikali katika kutoa haki.

Nyamoga alisema mafunzo hayo yakawe na manufaa kwa jamii kupitia utoaji ushauri, msaada wa kisheria, ulinzi wa haki za binadamu, pamoja na elimu ya Sheria kwa jamii.

Aidha, alisema Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) inatakiwa kushughulika kwa haraka kesi zinazokuja kwao ili haki itendeke.

Alisema kumekuwa na ukatili wa ajabu katika maeneo ya shule kwa wazazi kuwashawishi watoto wao waandike majibu ya uongo kwenye mitihani ili wasifaulu, ubakaji, mimba za utotoni. Pia alitaka semina hiyo ikawe chachu ya kutatua migogoro iliyopo pamoja na malalamiko yaliyopo juu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Amani haki na Msaada wa Kisheria Tanzania (PLAJC), Jaruo Karebe, alisema mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kushirikiana na wizara ya katiba na sheria.

Alisema baada ya uzinduzi wa mradi huo Aprili 12, mwaka huu, wameanza rasmi kutekekeza mradi wa kuimarisha upatikanaji wa haki jinai kwa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu katika Wilaya za Dodoma na Chamwino lengo likiwa ni kuangalia changamoto za kisheria.

Alisema mafunzo hayo yana lengo la kuwajengea uwezo wa ufahamu wa sheria.

Pia kukumbushana majukumu ya kila mdau kuhusu ulinzi wa wanawake na watoto, kuelimishana kuhusu usimamizi wa mashauri ya jinai na changamoto zake, namna ya kuzuia na kuchukua hatua ya ukatili wa kijinsia mashuleni.

Jukumu jingine ni kukumbushana wajibu wa shule na wadau katika kutokomeza ukatili wa kijinsia na kuelimishana mbinu za kuzuia na kutatua migogoro wa ardhi.

# Vijiji vinne vyapewa hatimiliki ya kimila kwa malisho

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HATIMILIKI za kimila zimetolewa kwa vijijini vinne vilivyotenga uwanda wa malisho ya mifugo wa pamoja wenye hekta 30,145.

Utoaji hatimiliki katika vijiji hivyo uliofanyika katika Kijiji cha Engong'ungare, Kata ya Kijungu, wilayani Kiteto ni wa kwanza hapa nchini ukiwa na lengo la kupanga matumizi ya ardhi na kuondoa migogoro kati ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine.

Hatimiliki hizo zilitolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mujibu wa sheria namba tano ya mwaka 1999 na Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magesa, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti.

Akikabidhi hati hizo, viongozi wa vijiji vya Olkitikiti, Lerug, Engong'ungare na Ngapapa kwa jina la (OLENGAPA), Mnyeti alisema eneo hilo lililotengwa kwa ajili ya malisho linatakiwa kutumika kwa kazi hiyo na atakayevunja makubaliano hayo atachukuliwa hatua.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mifugo, Prof. Olesante Ole Gabriel Zakaryya Kera, alisema wizara hiyo itaendelea na utaratibu wa kuendeleza maeneo hayo na kuhakikisha yanatumika kama yaliyotengwa.

Kera ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu katika Wizara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mifugo, alisema utengaji wa eneo la malisho umetumia gharama kubwa na rasilimali nyingi, hivyo kufikia makubaliano ya matumizi ya ardhi kwa pamoja na kusajili na hatimaye kupewa hatimiliki za kimila.

Akisoma ripoti ya Mradi, Afisa Mifugo na Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Lunonu Sigalla, alisema mradi huo pamoja na kupanga matumizi bora ya ardhi ni wa kwanza wafugaji kukubaliana kutenga eneo kwa ajili ya kufugia mifugo tu.

Alisema vijiji hivyo vimetenga uwanda wa malisho kwa kufuata ikilojia na Olkitikiti, imetenga hekta 17,167, Lerug 3,792, Ngapapa 575 na Engong'ungare 10,303, kwa ajili ya mifugo wakiwamo ng'ombe 20,525, mbuzi 31,3611 na kondoo 14,646 na wanyama wengine.

Dk. Sigalla alisema, wilaya ya Kiteto iliyokumbwa na migogoro ya wakulima na wafugaji, kuanzishwa kwa mradi huo wa kutenga maeneo kwa pamoja kwa ajili ya kufuga mifugo, pamoja na kupanga matumizi bora ya ardhi, malisho na shughuli nyingine za uzalishaji pia unalinda mazingira.



Baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilaya ya Momba, mkoa wa Songwe, wakiwa katika mafunzo ya maadili ya viongozi na matumizi ya simu za kisasa zitakazotumika kusajilia wanachama kwa njia ya kielektroniki, yaliyofanyika katika bonde la Kamsamba, mkoani humo jana. **PICHA: IBRAHIM YASSIN**

# Dk. Shein: Majadiliano ndiyo njia nzuri suluhu ya matatizo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema njia pekee ya kutatua matatizo ni kukaa pamoja na kujadiliana kwa busara na sio kutumia mapambano au mivutano isiyo na tija.

Akizungumza katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Duniani, alisema mfumo huo ndio unaotekelezwa kati ya Serikali na shirikisho la vyama huru vya wafanyakazi, kutokana na pande zote mbili kuelewa kwamba watu wote ni wamoja na wanategemeana katika kuleta maendeleo.

"Leo tuko katika karne nyingine, karne ambayo kwa mnasaba wa kudumisha amani na utulivu katika sehemu zetu tunazoishi, inatupasa tuzitatue changamoto zinazotukabili kwa utaratibu wa kukaa pamoja na kujadiliana kwa busara hadi kufikia ufumbuzi," alisema.

Alisema serikali inazingatia haja ya kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na vyama vya wafanyakazi sambamba na kuchukua hatua zinazostahiki kwa dhamira ya kuyashughulikia masuala ya wafanyakazi ili kuongeza kasi ya maendeleo, kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa jamii.

"Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa awamu zote saba za uongozi, imekuwa ikithamini na kutambua kuwa wafanyakazi ni nguzo kubwa na msingi wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Alisema ujumbe wa mwaka huu wa siku ya wafanyakazi unaosema 'kuimarika kwa uchumi wa taifa, kuendane na kuongezeka kwa maslahi ya wafanyakazi' utaendelea kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na serikali kadiri hali ya ukuaji wa uchumi utakavyozidi kuimarika.

Aidha, alisema kuimarika kwa amani na utulivu, kumeifanya Zanzibar kuwa katika karne mpya ambapo changamoto zote zinazojitokeza hutatuliwa kwa njia ya majadiliano na hatimae kupatiwa ufumbuzi. Alisema miongoni mwa hatua zilizochukuliwa kwa wafanyakazi baada ya kuimarika kwa uchumi ni pamoja na kuimarisha mazingira mazuri ya watumishi na kuyashughulikia maslahi yao.

Alisema kwa kutambua kwamba mazingira mazuri ya kufanyia kazi yanasaidia kuleta utulivu na kufanya kazi kwa umakini na hatimae kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi, serikali inaendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi za kisasa zinazokwenda na wakati.

Katika kuimarisha zaidi mfumo wa utumishi serikalini, alisema serikali imetunga na kuzifanyia mapitio sera, kanuni na sheria mbalimbali zinazohusiana na utumishi bora.

Aliwasisitiza viongozi na wafanyakazi kuzisoma sheria ili waweze kuzielewa na kufanyakazi kwa kuzingatia miongozo ya kisheria na kuleta ufanisi zaidi katika maeneo yao ya kazi.

Aliwataka wafanyakazi kuzingatia maadili ya utumishi kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanapatiwa huduma bora.

Aliwaasa wafanyakazi kuepuka vitendo vya ubadhirifu,wizi na uhujumu wa mali ya umma, rushwa, uzembe na unyanyasaji kwa wale wanaostahiki kuhudumiwa.

Naye Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Maudline Castico, aliwataka wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii na kujali uzalendo kwani utasaidia kuongeza pato la taifa.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Shirikisho la vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), Khamis Mwinyi Mohamed. alisifu juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kusimamia migogoro na haki za wafanyakazi na kutatua changamoto 21 kati ya 23 zilizowasilishwa.

# Watano mbaroni tuhuma za 'unga'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU watano wamekamatwa wakiwa na viwango tofauti vya dawa za kulevya Visiwani Zanzibar.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Thobias Sedoyeka, alisema hayo wakati akitoa taariza za matukio ya wiki kwa vyombo vya habari.

Alisema watu hao walikamatwa kufuatia operesheni iliyofanywa na polisi kuhakikisha mkoa huo unakuwa salama.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa na bangi katika maeneo mbali mbali ya Mkoa huo.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Salum Juma Hemedi (24), Ali Makame Adibu (29), Ali Rashud Ali (22), Mahamoud Khalid Mbarouk (21) na Ramadhan Abdalla Ali (18).

Alisema watuhumiwa watafikishwa mahakamani baada ya taratibu kukamilika.

Kamanda huyo aliwataka wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuwafichua wahalifu hasa wa dawa za kulevya ili kulinusuru taifa dhidi ya athari za dawa hizo.

# Vyakula sasa vyakaguliwa kwenye maghala, sokoni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TASISI ya Viwango Zanzibar, (ZBS) kwa kushirikiana na tasisi nyingine za serikali zinazofanya kazi za ukaguzi, zimeanza kufanya ukaguzi katika maghala na maduka ya vyakula katika masoko ya Zanzibar. Lengo la ukaguzi huo ni kuhakikisha wananchi wanakula vyakula vyenye ubora hasa katika kipindi hiki cha kuelekea mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Ukaguzi na udhibiti ubora wa tasisi hiyo, Suleiman Abdalla Mohammed, wakati akizungumza na Nipashe Mjini Zanzibar.

Alisema katika ukaguzi huo, wamechukua baadhi ya bidhaa kwa ajili ya kupimwa ili kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini zinakidhi matakwa ya viwango.

Alisema kuwa katika ukaguzi huo wamejikita zaidi katika bidhaa za vyakula ikiwamo tende, unga wa ngano, sukari, mafuta ya kula na bidhaa nyingine ambazo hutumika katika mwezi wa ramadhani.

Alisema, zoezi hilo litaendelea kwa muda wote ili kuhakikisha wananchi hawauziwi vyakula vilivyopita muda.

"Watakapoleta bidhaa ambazo hazikidhi matakwa ya viwango vyetu itaharibu nguvu kazi ya nchi ambayo inategemewa," alisema.

Hivyo, aliwaomba wafanyabiashara kuhakikisha bidhaa zao zinakaguliwa kabla hawajaziingiza sokoni. Naye msimamizi wa ghala la kuhifadhi chakula la kampuni ya Yasir Provision S&S, Adil Yaqub Othman, alisema hakuna uhakika wa upatikanaji mchele kwa mwezi wa Ramadhani, kutokana na tatizo la usafiri.

Alisema mchele unapotoka Pakistan unachukua siku 10 kufika bandari ya Mombasa, lakini tatizo ni kutoka Mombasa hadi Zanzibar, ambapo inachukua zaidi ya siku 60 hadi kupakuliwa, kutokana na tatizo la usafiri na ufinyu wa nafasi bandarini.

Hata hivyo, alisema kuanzia Julai huenda bei ya mchele ikapanda kutokana na gharama za usafiri kuongezeka.

# HABARI KIMATAIFA

## Rais arejea baada ya kukimbizwa na nyoka

**MONROVIA,** Liberia

RAIS wa Liberia, George Weah, amerejea tena kazini zikiwa zimepita wiki mbili tangu alipoikimbia ofisini yake baada ya nyoka wawili kuingia katika ofisi yake.

Baada ya kutokea kwa tukio hilo, Jengo hilo lilitakiwa kusafishwa vizuri kwa kemikali ya kuua nyoka kabla rais kurejea ofisini kwake.

Mmoja wa watu wa kwanza kumtembelea Rais Weah katika ofisi yake alikuwa ni Makamu rais wa zamani, Joseph Boakai, aliyeshindwa na Weah katika uchaguzi wa urais wa mwaka 2017. Muda mfupi baada ya kurejea ofisini, Rais Weah alizungumzia juu ya juhudi za serikali yake za kulinda misingi ya demokrasia na kuwavutia wawekezaji wa kigeni ili kuinua uchumi.

Rais Weah amekuwa akifanyia kazi zake katika ofisi iliyopo ghorofa ya sita ya jengo la Wizara ya mambo ya nje tangu jengo jirani na ofisi yake lilipoungua kwa moto mwaka 2006.

Nyoka wawili weusi ambao walitoka kwenye shimo lililokuwa sehemu ya mapokezi ya jengo la ghorofa sita walikwenda nyuma ya jengo ambalo Rais Weah afanyia kazi, lakini wananchi waliwaua.

Baada ya tukio hilo maafisa wa polisi na maafisa wa usalama wa rais walionekana wakiyalinda makao ya Rais Weah yaliyopo Mji Mkuu wa Monrovia. **BBC**

## Upinzani Afrika Kusini wapaza sauti dhidi ya ANC

**JOHANESSBURG,** Afrika Kusini

WANANCHI wa Afrika Kusini wanajiandaa kumchagua rais wao mpya ndani ya wiki moja.

Uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Jumatano wiki ijayo, huku Rais anaye maliza muda wake, Cyril Ramaphosa anapewa nafasi kubwa ya kushinda. Kulingana na uchunguzi wa awali chama tawala cha ANC kinaongoza kwa asilimia 50 ya kura zilizopigwa.

Chama kikuu cha upinzani cha Democratic Alliance kinasema, iwapo kitashinda uchaguzi huo kitatekeleza maoni ya rais wa kwanza wa taifa hilo, Nelson Mandela, aliyetaka nchi ya Afrika Kusini kumjumuisha kila mmoja.

Uongozi wa chama hicho unasema kuwa sera zao zinaangazia yale aliyoyaamini Mandela na unashtumu chama tawala cha ANC kinachopewa nafasi kubwa kwenye uchaguzi kuwa kimeshindwa kusimamia maoni ya kiongozi huyo wa zamani.

Jumatano ya wiki iliyopita katika uwanja wa Alexandra Stadium, Malema alisema: "ANC ilifanya nini? Hakuna! Walijihusisha tu na kuiba fedha. Hii ndiyo sababu chama cha EFF kinasema kwamba ni lazima tuwanyang'anye mashamba wakulima bila fidia na kuwapa wenyeji wa Alexandra ili waweze kujenga nyumba zao". **RFI**

# Mfalme amuoa mlinzi wake, amtawaza kuwa malkia

**BANGKOK,** Thailand



**Mfalme Vajiralongkorn ameamua kumpandisha cheo Generali Suthida na kuwa Malkia na atakuwa na cheo cha kifalme na hadhi kama sehemu ya familia ya kifalme.**

MFALME wa Thailand, Maha Vajiralongkorn, amemuoa Naibu Mkuu wa kikosi cha walinzi wake Suthida na kumpa cheo cha malkia.

Tangazo hilo la kushitukiza limetolewa huku sherehe za kutawazwa kwake zikitarajiwa kuanza Jumamosi, wakati atakapochukua wadhfa wake.

Mfalme Maha Vajiralongkorn, mwenye umri wa miaka 66, alikuwa mfalme kikatiba baada ya kifo cha baba yake mwaka 2016. Hadi sasa Mfalme Maha ameshawataliki wanawake mara tatu na ana watoto saba.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa: "Mfalme Vajiralongkorn ameamua kumpandisha cheo Generali Suthida na kuwa Malkia na atakuwa na cheo cha kifalme na hadhi kama sehemu ya familia ya kifalme." Malkia Suthida alikuwa ni mpenzi wa muda mrefu wa Mfalme Vajiralongkorn na amekuwa akionekana hadharani pamoja nae kwa miaka mingi, ingawa mahusiano yao haukuwahi kuthibitishwa rasmi.

Picha kutoka katika sherehe za harusi zilionyeshwa moja kwa moja kwenye vituo vya televisheni vya Thailand Jumatano, ambapo watu mbalimbali wa familia za kifalme na washauri wa ufalme walihudhuria.

Mfalme Maha alionekana akimmwagia maji ya baraka Malkia Queen Suthida kichwani. Baadae wawili hao walisaini cheti cha ndoa.

Mnamo mwaka 2014 Vajiralongkorn alimteua Suthida Tidjai, ambaye alikuwa mhudumu wa zamani wa Thai Airways kuwa Naibu kamanda wa kikosi cha walinzi wake, alimpandisha cheo kuwa Generali kamili jeshini Desemba 2016.

Mfalme aliyetangulia, Bhumibol Adulyadej, alitawala kwa miaka 70 na kuwa mfalme pekee aliyetawala kwa muda mrefu zaidi duniani, alifariki dunia mwaka 2016. **BBC**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi (kushoto), Sergei Lavrov na Mike Pompeo wa Marekani. **PICHA: ALLIANCE**

# Marekani, Urusi zatunishiana misuli

**CARACAS,** Venezuela

MZOZO wa kuwania madaraka nchini Venezuela kati ya Rais Nicolas Maduro na Spika wa Bunge, Juan Guaido, unazidi kufukuta huku Urusi na Marekani zikichukuwa nafasi yao kwenye taifa hilo la Amerika ya Kusini.

Mei mosi Guaido aliitisha tena maandamano ya umma kwenye mitaa ya Mji Mkuu Caracas, lakini waandishi wa habari walioko huko walisema vyombo vya usalama vimefanikiwa kudhibiti hali ya usalama na wengi wa wanajeshi hawakuitikia wito wake wa kuungana na wenzao walioasi kumpindua Rais Maduro.

Akiwahutubia wafuasi wake, Rais Maduro alikanusha vikali kauli ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, kwamba rais huyo alikuwa tayari kuachia madaraka na kukimbilia nchini Cuba.

Rais Maduro alisema viongozi wa Marekani walikuwa wanadanganywa na wapinzani wake ili kuwasaidia njama ya kumuondoa, lakini hilo lisingelifanikiwa.

"Jaribio lile la mapinduzi ambalo lilifanyika jana, upuuzi huo wa kupindua uliongozwa moja kwa moja kutoka Ikulu ya Marekani, na John Bolton. Hicho ndicho ninachokilaani na kutaka hatua hizi haramu na jaribio la mapinduzi dhidi ya demokrasia ya Venezuela lichunguzwe ndani ya Marekani," Aliwaambia wafuasi hao.

Kikosi maalumu cha ulinzi wa Rais Maduro kiliwatawanya waandamanaji waliokuwa wamekataa kuondoka mitaani hapo jana, kikitumia mabomu ya kutoa machozi, ambapo mtu mmoja alijeruhiwa.

Makundi ya haki za binaadamu yalisema mwanamke mmoja alifariki dunia wakati akifanyiwa upasuaji kufuatia kupigwa risasi kichwani mjini Caracas.

Mkwamo huu wa kisiasa nchini Venezuela unaongeza mzozo kati ya Marekani na Urusi, zinazotuhumiana kuingilia mambo ya ndani ya taifa hilo ambalo ni mwanachama wa Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta kwa wingi duniani, OPEC.

Utawala wa Rais wa Marekani, Donald Trump umeiwekea vikwazo serikali ya Maduro na imekataa kuivamia Venezuela kijeshi, licha ya kupendekeza kuwapo kwa kipindi cha mpito kwa njia ya amani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, jana alikiambia kituo cha Fox Business Network kuwa matumizi ya jeshi yanawezekana.

Rais wa Urusi, Sergei Lavrov, alisema kuwa hatua yoyote zaidi ya uchokozi nchini Venezuela haitavumiliwa. **DW**

# Waipa serikali siku 21 uchaguzi mitaa

**Na Mary Geofrey**

VYAMA 10 vya upinzani vinavyoshirikiana kisiasa nchini, vimeitaka serikali kutoa kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa ndani ya wiki tatu.

Vyama hivyo ni pamoja na ACT-Wazalendo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Chama cha Ukombozi wa Umma (Chauma), Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC).

Vingine ni Chama cha Kijamii (CCK), Chama cha Democratic Party (DP), Chama cha NCCR MAGEUZI, National League for Democracy (NLD) na Chama cha United People's Democratic Party (UPDP).

Akizungumza katika mkutano wa pamoja wa vyama hivyo vya upinzani uliofanyika jana jijini Dar es Salaam, Katibu wa CCK, Renatus Muabhi, alidai habari walizonazo ni kuwa kanuni hizo zimeshatoka lakini serikali imeshindwa kuzisambaza kwa maslahi yake binafsi.

Muabhi alidai lengo la serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni kujiwekea mbinu mkakati za kushinda katika uchaguzi ujazo.

"Tumepata fununu kwa kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa zimeshatoka, tunachoimba serikali itoe kanuni hizo ili vyama vya upinzani wazisome kabla ya kuanza kwa uchaguzi na tunatoa wiki tatu kwa serikali wawe wameshazitoa," Muabhi alisema.

Alieleza kuwa endapo serikali haitatoa kanuni hizo ambazo zitawapa mwongozo wa kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, watakuja na uamuzi mgumu ambao ni maazimio ya vyama 10 vya upinzani.

"Kama wiki tatu zitamalizika na serikali haijatoa kanuni hizo za uchaguzi ili tufahamu kanuni za uchaguzi, tutakuja na maamuzi mazito ambayo hatujawahi kuyafanya," alisema.

Mwenyekiti wa Chauma, Hashim Rungwe, alidai CCM kimejipanga kutaka kushinda katika uchaguzi huo ndiyo sababu ya kuzuia kanuni hizo.

## Waandishi 1,300 wauawa miaka 24

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JUMLA ya waandishi wa habari 1,307 waliuawa kati ya mwaka 1994 na 2018 wakati wakitekeleza majukumu yao ya kikazi katika nchi mbalimbali Duniani.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa kitengo cha habari cha Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), Nancy Kaizilege, wakati akitoa mada kwenye maadhimisho ya siku ya Uhuru wa Habari yanayofanyika Jijini Dodoma.

Kaizilege alisema ripoti ya shirika hilo ilidai idadi hiyo ya wandishi wa habari waliuawa kwa kipindi cha kutoka mwaka 1994 hadi 2018 katika nchi mbalimbali wakati wakitekeleza majukumu yao.

"Tishio hili linatufanya tuwe macho wakati wote, lazima tusimame pamoja, tushikamane ili kulinda uhuru wa kujieleza na usalama wa waandishi wa habari," alisema.

Alisema ripoti hiyo iliyotolewa na UNESCO inaonyesha kuwa waandishi wa habari 99 waliuawa katika kipindi cha mwaka 2018 wakitekeleza majukumu yao maeneo mbalimbali.

Kaizilege alisema hali hiyo ya kutokujali uhalifu dhidi ya wandishi wa habari ni tishio linaloathiri jamii zote kukosa haki yao ya kupata habari.



Mmoja wa abiria wanaotumia programu ya Bolt, akipata huduma kutoka kwa dereva bodaboda, baada ya kampuni ya Bolt kuzindua kitufe cha dharura (SOS), jijini Dar es Salaam jana, kwa lengo la kuimarisha usalama wa madereva wanapokutana na hatari. **NA MPIGAPICHA WETU**




## Watupwa jela miaka 150

**Na George Marato,** MUSOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara, imewahukumu kifungo cha miaka 150 watu wanne kati ya saba walioshtakiwa kwa makosa manne likiwamo la unyang'anyi wa Sh. milioni 20 kwa kutumia silaha.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 83 ya mwaka 2016, washtakiwa walikuwa wanakabiliwa na mashtaka mengine ya kujeruhi, kumiliki silaha na risasi kinyume cha sheria na kupatikana na bunduki, washtakiwa wawili wakiachiwa huru na mmoja kufariki dunia akiwa mahabusu.

Walidaiwa kufanya kosa hilo Desemba 12, 2015 majira ya saa 12:30 jioni na kufanikiwa kupora kiasi hicho cha fedha, mali ya Juma Kisyeri wakitumia bunduki aina SMG yenye namba 10353 ikimilikiwa na Shukuru Alani kinyume cha Kifungu Na. 20 cha Sheria ya Umiliki na Udhibiti wa Silaha.

Akisoma hukumu ya kesi hiyo iliyochukua zaidi ya saa tatu jana, Hakimu wa mahakama hiyo, Stanley Mwakihaba, alisema kulingana na ushahidi ambao ulitolewa mahakamani hapo na mashahidi 27 wa upande wa mashitaka, mahakama imejiridhisha pasi na shaka kuwa watu hao walihusika katika tukio hilo.

Kwa sababu hiyo alisema mahakama hiyo inawahukumu kutumikia kifungo cha miaka 35 kila mmoja, Bwire Julius, Reiner Fabian na Ally Pima huku Shukuru Alan akifungwa kifungo cha miaka 45 baada ya kukutwa na kosa la kumiliki silaha hiyo, risasi 12 na sare za Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Walioachiwa huru ni marehemu Godwill Samwel na wengine Robert Manyama na Khamis Kome baada ya ushahidi kushindwa kuwatia hatiani.

Hata hivyo, mahakama hiyo iliamuru mali na fedha za waliohukumiwa kifungo hicho na kukutwa nazo wakati wakikamatwa, kutaifishwa ili kumfidia mlalamikaji Juma Kisyeri huku bunduki na risasi hiyo kuwa mali ya serikali kuanzia tarehe ya hukumu.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KADI YA GARI IMEPOTEA

**ABDULFATAH SALIM SALEH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa T367 CJC aina ya TOYOTA NOAH. CHASSIS NAMBA.AZR600207075 na ENGINE NAMBA. 1AZ213321.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Polisi.

**KIT/RB/2542/2019**

115208902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 63/2019**

Ombi la ALLY MWINYIHAMISI OMARY kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu HALIMA ALLY

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 29/4/2019

115208802

---

**JAUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAM A**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya **MWANZO DODOMA MJINI**
Usimamizi wa mirathi **NA. 24/2019**

Ombi la **MAKATA SHABANI** kuteuliwa Msimamiliz wa mirathi ya marehemu **SHABANI SELEMANI KANDA**

Kwa yeyote anayehusika … **TANZANIA -BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 13/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyoupo mahakamni waweza kukaguliwa

**Tarehe 29/04/2019**

215207902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 61/2019**

**Ombi la EDWARD D. HERMAN kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu GRACE J. MGAYA**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 25/4/2018**

215208101

---

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**NADEEM NASIR** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa **T753 CTN** aina ya SUZUKI CARRY.

CHASSIS **NAMBA.DD51T-581610**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Polisi.

**TAN/RB/3626/2019**

215208202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya wilaya ya Dodoma Mjini**
**Madai na. 22/2019**
**Mdai Hamisi Amri**
**MDAIWA Hasfa Juma**
**Kwa Hasfa Juma-Mwandiga Kigoma**
**Mwenyekiti wa Mtaa Mwandiga**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA TALAKA**

Hivyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya J/Tano Tarehe 6/5/2019saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itadhibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshundwa /mmeshindwa .

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 29/4/2019

215207802

---

**JAUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAM A**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya MWANZO DODOMA MJINI

Usimamizi wa mirathi NA28/2019
Ombi la **FRIDA EDWARD KISHALULI** kuteiliwa Msimamiliz wa mirathi ya marehemu **SHUKURU ANANGISYE MLWAFU**
Kwa yeyote anayehusika …**TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 9/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyoupo mahakamni waweza kukaguliwa

Tarehe 24/04/2019

215208002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**
**SHAURI LA MIRATHI NA. 7/2018**
**Maombi ya barua za usimamizi wa Mirathi ya**
**AHMED S. GHOTH BAWAZIRI ………..MAREHEMU**

**NA**

**SAID AHMED GHOTH……………MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jadal kama wananona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yeyotr kuhusu maombo haya yawe yameandikishwa mnano au kabla ya terehe 10/6/2019

Imewasilishwa leo 29/4/2019

215208302

---


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LUKAKU HAJUI HATMA YAKE UTD



**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Romelu Lukaku, ameonyesha wasiwasi wake wa kubaki kwenye timu hiyo baada ya kusema hana uhakika wa nafasi yake katika msimu ujao.

Mshambuliaji huyo ameshindwa kufanya vizuri katika kikosi cha Manchester United msimu huu na amekuwa akichukiwa sana na mashabiki wa timu hiyo.

Hivi karibuni taarifa zilitoka kuwa anawindwa na timu kadhaa kubwa ikiwamo Juventus na Inter Milan zote za Italia.

Wiki iliyopita alinukuliwa akisema kuwa atafurahi kama siku moja atacheza kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 25 bado ana mkataba wa miaka mitatu na United.

"Mimi sijui kama nitakuwa hapa msimu ujao, lakini ieleweke kuwa sipo hapa kufuatilia tetesi zinasemaje.

"Naamini kuwa bado msimu wa ligi haujamalizika na kuna kazi kubwa sana, natakiwa kuifanya ndiyo naweza kuwaza mambo mengine."

Lukaku kwenye michuano yote msimu huu amefanikiwa kucheza michezo 45 na amefunga mabao 15 huku akifanikiwa kutoa pasi nne za mabao.

# Benitez: Liverpool wasitarajie mteremko

**LONDON,** England

RAFAEL Benitez ameionya klabu yake ya zamani Liverpool kutotarajia huruma wakati watakapokutana kwenye mchezo wa Ligi Kuu England na Newcastle United.

Huku mbio za kuwania ubingwa wa Ligi hiyo zikielekea mwisho, kikosi hicho cha Jurgen Klopp kipo nafasi ya pili na kitavaana na Newcastle Jumamosi kikijaribu kurudi kileleni mwa msimamo.

Lakini Benitez, ambaye aliiongoza Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA katika kipindi chake cha miaka sita, alisema kikosi chake hakina mpango wa kuisaidia klabu yake hiyo ya zamani.

"Tutafanya kile tunachotakiwa kufanya na kujaribu kushinda mchezo," alisema Benitez wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo huo.

"Tutacheza nyumbani mbele ya mashabiki wetu na tutajaribu kucheza kwa ubora wetu. Tutakuwa kwenye ubora wetu.

"Unatakiwa kukumbuka kwamba timu zote zina mechi 38 na zinatakiwa kucheza kwa uwezo wetu.

"Ni majukumu yetu kuangalia kila mchezo uliopo mbele yetu na hatutakuwa na nafasi ya kuangalia nafasi ya timu nyingine zaidi ya sisi wenyewe tu."

Newcastle ipo nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu na imejiweka kwenye nafasi ya kubaki kwenye ligi hiyo msimu huo.






# Wright: Solskjaer achana na De Gea

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anatakiwa kutokuwa mwoga wa kufanya maamuzi makubwa kwa kumuacha golikipa, David De Gea kwa mechi mbili za mwisho za Ligi Kuu England, mshambuliaji wa zamani wa England, Ian Wright amesema.

De Gea amefanya makosa makubwa kwenye mechi za hivi karibuni, likiwamo moja liliwaruhusu Chelsea kusawazisha kwenye sare ya 1-1 na kuifanya United kufifisha matumaini ya kumaliza kwenye nne bora.

Solskjaer alimtetea De Gea kuwa ataendelea kucheza kwenye mechi mbili za mwisho dhidi ya Huddersfield Town na Cardiff City lakini Wright anaamini kocha huyo raia wa Norway kuchukua maamuzi tofauti.

"Kama yeye (Solskjaer) anataka kuonyesha kwamba ana uwezo, anatakiwa kufanya maamuzi bila woga, anatakiwa kumuacha nje," amesema Wright akiiambia BBC Radio 5.

"Kocha anatakiwa kuelezea kwa ukweli kabisa sababu ya kumuacha ili aweze kufanya maamuziyatakayoisaidia klabu na si vinginevyo," alisema Solskjaer."

Mkataba wa sasa wa De Gea ulikuwa unatarajiwa kumalizika mwaka huu kabla ya United kuongeza kwa mwaka mmoja zaidi, lakini bado ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuondoka katika Klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu hapo Old Trafford.

## HABARI MICHEZO

# KLOPP: MESSI SIO MTU WA KAWAIDA




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amemwagia sifa, Lionel Messi na kusema kwamba sio mchezaji wa kawaida.

Messi alifunga mabao mawili wakati Barcelona wakiambulia kichapo cha mabao 3-0 katika mchezo wa kwanza wa hatua ya Nusu Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi Jumatano kwenye Uwanja wa Camp Nou.

"Katika wakati huu yeye hawezi kushindwa, tusingeweza kuuzuia mpira wa adhabu ndogo na tulijikuta hatuna namna," amesema Klopp mara baada ya mchezo huo.

"Goli la pili labda sio lilelo bora sana katika kazi ya Lionel Messi, lakini inaonyesha ujuzi wake.

"Mbali na kwamba nilifurahi jinsi tulivyoizuia timu nzima ya Barcelona. Mimi nimewakubali.

"Tulicheza vizuri, nilijua kabla ya kuwa Lionel ni mchezaji wa daraja la juu duniani na sasa nimeona tena mimi sina cha kushangaa."

Liverpool sasa watakuwa na kazi ya ziada ya kupindua matokeo katika mchezo wa marudiano utakaopigwa Jumanne ijayo.



# Casillas augua moyo, akimbizwa hospitali

**LISBON,** Ureno

GOLIKIPA wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania na Real Madrid, Iker Casillas alilazimika kukimbizwa hospitalini baada ya kupata mshutko wa moyo ghafla akiwa mazoezini juzi.

Casillas akiwa katika mazoezi na timu yake ya FC Porto ya nchini Ureno, alipata matatizo ya mshtuko wa moyo na kulazimika kukimbizwa hospitali kwa ajili ya kupatiwa huduma zaidi.

Baada ya kukimbizwa hospitalini Casillas ambaye alitumiwa jumbe za faraja na wachezaji mbalimbali wakiwamo aliocheza nao Real Madrid kama Gareth Bale na Sergio Ramos, kwa sasa anaendelea vizuri na hali yake imeimarika.

Taarifa ya Klabu ya Porto kupitia kwenye tovuti yake ilisema kwamba, Casillas anaendelea vizuri na hali yake imeimarika.

"Casillas kwa sasa anendelea vizuri na afya yake imeimarika kwa kiasi kikubwa," ilisema taarifa ya Klabu ya FC Porto. Casillas mwenye umri wa miaka 37 alijiunga na FC Porto mwaka 2015 baada ya kuichezea Real Madrid kwa miaka zaidi ya 15.

# Semenya ashindwa kesi yake

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MWANARIADHA wa kike wa Afrika Kusini, Caster Semenya ameshindwa katika kesi muhimu dhidi ya shirikisho la riadha duniani, hii ikimaanisha kuwa shirika hilo litaruhusiwa kudhibiti viwango vya homoni za wanariadha wa kike.

Mahakama ya usuluhishi wa migogoro michezoni (Cas) imekataa kesi ya Afrika Kusini ya kupinga sheria mpya za IAAF.

Lakini Cas ilisema kuwa ilikuwa na "hofu kubwa juu ya utekelezwaji wa baadaye" wa sheria hizo mpya. Semenya, mwenye umri wa miaka 28, alisema sheria hizo "si za haki " na kwamba alitaka "kukimbia kama nilivyo, jinsi nilivyozaliwa."

Sasa mshindi huyo wa Olimpiki, dunia na mashindano ya Jumuiya ya Madola kwa mita 800 pamoja na wanariadha wengine wenye jinsia zaidi ya moja (DSD), watalazimika kupata matibabu ili kushiriki mashindano ya kuanzia mbio za mita 400, au wabadili mbio.

Cas ilibaini kuwa sheria zilizokuwapo za wanariadha wenye DSD zilikuwa ni za kibaguzi -lakini kwamba ubaguzi huo ulikuwa "muhimu, wa kueleweka na wa uwiano kwa ajili ya kulinda maadili ya wanariadha wanawake ".

Hofu kwamba wanariadha wanaweza kukiuka masharti ya viwango vya homoni za kike vilivyowekwa na IAAF; Maswali kuhusu faida za viwango vya juu homoni za jinsia tofauti wanazozipata wakimbiaji wa mita 1500 na maili.

Cas imeitaka IAAF kuangalia uwezekano wa kuchelewesha utekelezwaji wa sheria hizo kwa wanariadha wanaokimbia katika matukio ya mita 1500 na maili moja hadi pale ushahidi utakapopatikana.

Semenya hatatakiwa kupunguza viwango vyake vya homoni za (testosterone) kama alikamilisha hilo katika mbio za Diamond Ligi mjini Doha Ijumaa. Matokeo ya utafiti wa jinsia uliofanywa miaka 10 iliopita bado hayajatangazwa hadharani, licha ya kwamba vyombo vya habari vimetuhumu kwamba ana sifa za kike na kiume ikiwamo kiwango kikubwa cha homoni za kiume.

Shirikisho la riadha duniani IAAF lilipendekeza sheria kuzuia viwango vya homoni hiyo ya testosterone inayoruhusiwa kwa wanariadha wanawake katika mashindano ya mita 400. Semenya alipinga uamuzi huo mahakamani ya kutatua mizozo katika michezo.



DON ZA A
MA AZET YA A




# MADRID YAJITOSA KUMWANIA JOVIC

## Straika Mserbia anayewindwa na vigogo Ulaya lakini dau lake likiwashtusha...

**MADRID,** Hispania

KAMA Chelsea itafanikiwa kusonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Europa yanayoendelea wiki hii, basi itaifanya klabu hiyo kuingia kwenye soko la usajili ambao utawaimarisha kuelekea kwenye mchezo wa marudiano.

**Klabu hiyo maarufu kwa jina la The Blues na moja ya timu kubwa duniani inahusishwa na mipango ya kumwania straika Mserbia Luka Jovic (21), ambaye anatarajia kuiongoza timu yake ya Eintracht Frankfurt leo katika mchezo wa kwanza wa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Europa.**

Jovic ametajwa kuwa mmoja wa wachezaji hatari katika Ligi ya Bundesliga akiwa bora kwenye msimu huu, ameifungia Frankfurt mabao 25 na kuchangia rekodi ya mafanikio mbalimbali klabu hiyo kwa siku za hivi karibuni.

Kiwango chake cha juu kimeifanya Eintracht kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na pia kufanya vema kwenye michuano ya Ligi ya Ulaya, na mabao yake aliyofunga katika mechi dhidi ya Inter Milan na klabu yake ya zamani ya Benfica yaliwapeleka Wajerumani hao kwenye hatua ya Nusu Fainali ya Ligi ya Europa msimu huu.

Straika huyo sasa amekuwa mmoja wa wachezaji wanaowindwa na klabu kongwe kama Barcelona, Bayern Munich na Real Madrid nayo imejitosa kwenye vita hiyo. Miaka miwili iliyopita, Jovic alijiunga na Frankfurt kwa mkopo akitokea Benfica kama mchezaji ambaye hakuwa na thamani, huku klabu hiyo ya Ureno ikifikia uamuzi wa kumwacha kwa amani ikidai kwamba hakuwa na uwezo mzuri kama mchezaji.

Jovic hakuwa hata kwenye kikosi cha akiba alipokuwa Lisbon, na hata mwaka wake wa kwanza akiwa hapo Frankfurt, alishindwa kuonyesha kiwango chake kwa kushawishi kocha ampange, na chini ya Kocha, Niko Kovac, alicheza kwa muda mchache katika msimu uliopita, na alibakia kuwa mchezaji asiyekuwa na mchango hadi ilipofikia Machi mwaka jana.

'Nilipotua hapa, nilibaini kuwa mchezaji ambaye ana kipaji, mchezaji ambaye huwezi kuamini ni hatari," alisema Hutter akimwelezea Jovic mwezi uliopita. Siwezi kusema kwa nini kipaji chake hakikuonekana alipokuwa Benfica.'

Hakuna shaka yoyote na kiwango cha Jovic. Ni mshambuliaji mwenye uwezo na anayeweza kuonyesha mashambulizi akitokea kati. Kocha Mserbia Mladen Krstajic alimfananisha na nyota wa Barcelona, Luis Suarez.

## ZISIKUPITE

### ERIKSEN ANUKIA MADRID

KIUNGO wa Tottenham, Christian Eriksen, amefikia makubaliano ya awali ya kujiunga na klabu ya Real Madrid ya Hispania katika kipindi cha majira ya joto. ***(AS)***

### SPURS KUIKAMIA MADRID

INASEMEKANA mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, atahitaji kiasi cha pauni milioni 128 kwa ajili ya kumuuza kiungo huyo wa kimataifa wa Denmark, Christian Eriksen. ***(Mirror)***

### UNITED YATUA URENO

MANCHESTER United wameanza mbio za kuwawinda nyota wawili wa Ureno, Mshambuliaji wa Benfica, Joao Felix na kiungo wa Sporting, Bruno Fernandes, 24. ***(London Evening Standard)***

### SOLSKJAER AMTAKA PHELAN

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anaitaka klabu hiyo imteue, Mike Phelan kuwa Mkurugenzi wa Ufundi wa kwanza wa klabu hiyo. ***(Times - subscription required)***

### OZIL: NINAIPENDA ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal, Mjerumani Mesut Ozil (30), amesisitiza ana furaha na anataka kuendelea kubaki ndani ya klabu hiyo katika msimu ujao. ***(Sky Sports)***

### MUSONDA KUREJEA VITESSE

KIUNGO wa Chelsea na Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21 ya Ubelgiji (U-21), Charly Musonda, ana matumaini ya kurejea kwa mkopo katika klabu ya Uholanzi ya Vitesse msimu ujao. ***(Inside Futbol)***

### UNITED KUMJARIBU TUANZEBE

MANCHESTER United ipo tayari kumpa nafasi kuonyesha uwezo wake beki mwenye umri wa miaka 21, Axel Tuanzebe ambaye anayecheza kwa mkopo katika klabu ya Aston Villa, ili kumwangalia kama ataweza kuingia kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo. ***(Mail)***

### PALACE YAJIPANGA

MWENYEKITI Crystal Palace na mmoja wa wamiliki wa timu hiyo, Steve Parish amewahakikishia mashabiki kuwa "hatapumzika" mpaka atakapohakikisha ujenzi wa jukwaa Selhurst Park litakalobeba watu zaidi ya 34,000 linakamilika. ***(London Evening Standard)***

### POCHETTINO SOKONI

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino, anaonekana atakiimarisha kikosi chake kwa kusaka wachezaji wanaowaniwa pia na majiraji zake kwenye kipindi cha majira ya joto.***( Telegraph)***

### PAULISTA AIPANIA ARSENAL

BEKI wa zamani wa Arsenal ambaye anaichezea Valencia, Gabriel Paulista, amesema kuwa hana chochote cha kupoteza wakati timu hizo zitakapokutana katika mechi ya nusu fainali ya Ligi ya Europa. ***(Independent)***

### MESSI AMBEBA COUTINHO

STRAIKA wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi (31), amewataka mashabiki kuacha kumzonga mchezaji mwenzake wa timu hiyo, Mbrazil Philippe Coutinho (26), kwa kumwita ni mtu mbaya. ***(Marca)***

HUZUNI 1942 - 2019

# Wadau wa michezo wamlilia Dk. Mengi

Na Somoe Ng'itu

● ● ● Waeleza bado mchango wake ulikuwa unahitajika katika kuinua michezo...

WADAU mbalimbali wa michezo nchini, wamepokea kwa huzuni taarifa za kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP na Mlezi wa Timu ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Dk. Reginald Mengi, kilichotokea usiku wa kuamkia jana katika Umoja wa Falme za Kiarabu, (U.A.E).

**Marehemu Dk. Mengi alikuwa ni mlezi wa Serengeti Boys na alitoa mchango mkubwa katika kufanikisha maandalizi ya timu hiyo iliyokuwa mwenyeji wa Fainali za Afrika za Vijana (AFCON U-17) ambazo zilimalizika hapa nchini Jumapili iliyopita.**




Aliyekuwa mlezi wa Timu ya Serengeti Boys, Dk. Reginald Mengi (kulia), akiwa na shabiki wa timu hiyo, Ikwizi Kicheko kutoka Manyara. **PICHA: MAKTABA**

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kupitia Rais, Wallace Karia, ilisema kuwa wamepokea kwa mshtuko na majonzi taarifa za kifo hicho cha Dk. Mengi ambaye alikuwa mdau mkubwa wa michezo na alifanya kazi karibu na shirikisho hilo. Karia alisema katika taarifa yake kuwa Dk. Mengi alikuwa na mchango mkubwa katika mpira wa miguu na mchango wake bado ulikuwa unahitajika.

"Nimepokea kwa mshtuko mkubwa taarifa za msiba wa mlezi wetu wa Serengeti Boys, Dk. Reginald Mengi, sote ni mashahidi kwa namna alivyojitolea katika mpira wa miguu kuanzia ngazi ya klabu mpaka katika timu za taifa, hakika mchango wake ulikuwa bado unahitajika," alisema Karia katika taarifa yake.

Aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Davis Mosha, alisema kifo cha Dk. Mengi ni pigo kwa klabu hiyo na wanamichezo wote nchini.

Mosha alisema kuwa marehemu, Dk. Mengi ambaye alikuwa ni mwanachama wa Yanga, alikuwa akipenda kuona klabu na timu za taifa zinafanya vema katika mashindano mbalimbali waliyokuwa wanashiriki ndani na nje ya Tanzania. Alisema pia mfanyabiashara huyo maarufu Tanzania alikuwa ni rafiki na ndugu wa watu wa rika na kabila tofauti.

"Ni majonzi makubwa na wingu la giza kukupoteza mzee wetu, mshauri wangu, rafiki yangu Dk Mengi, tutakukumbuka daima, umeacha alama kubwa duniani, tulikupenda sana kwa ujasiri wako kama mtu uliyethubutu na ukaweza. Tumejifunza vingi kupitia kwako. Kapumzike kwa amani na Mungu akupokee na mwanga wa milele ukufariji pale roho yako itakapokua. We will miss you Daddy (tutakukosa Baba," alimaliza Mosha.

Kiungo wa kimataifa wa Simba, Haruna Niyonzima, aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwa kuwa marehemu, Dk. Mengi alikuwa ni mmoja wa wapambanaji na hakupenda kuona kijana anashindwa kufikia ndoto zake. Niyonzima alisema kuwa kifo ni safari na sasa muda wa mfanyabiashara huyo umefika, hivyo anamwombea apumzike kwa amani.

'Wewe ulikuwa ni kioo cha wapambanaji, pumzika kwa amani Mzee Mengi, dunia hii sio nyumbani kwetu, vitu ulivyovifanya kwa jamii inayotuzunguka ni ishara sahihi kuwa ulibarikiwa. Ulikuja kuishi kwa malengo maalumu. Kauli mbiu yako ya I CAN, I MUST I WILL itabaki daima katika kumbukumbu zetu. Mungu tunaomba uipe nguvu na faraja familia yako katika kipindi hiki kigumu," alisema kiungo huyo wa zamani wa Yanga na APR ya Rwanda.

**Tunajua kazi yako haina makosa, lakini turuhusu kwa unyenyekevu tumlilie baba na rafiki yetu mpendwa, wenyewe tulikuwa tukimwita Chairman. Pumzika kwa amani baba Mengi.**

Mdau mwingine wa soka aliyejitambulisha kwa jina la Frank Gwaluma, aliiambia gazeti hili kuwa anakumbuka mwaka 1994, marehemu, Dk. Mengi alisaidia mashabiki wa mchezo huo kuangalia mechi za Fainali za Kombe la Mataifa Huru sasa AFCON kupitia luninga kubwa iliyoandaliwa kwenye viwanja vya Mwanza Community Centre.

"Nakumbuka mwaka 1994 aliweka "screen" kubwa pale Mwanza Coomunity Center, tukawa tunaenda kuangalia bure mechi za Kombe la Mataifa Huru Afrika, angalia enzi hizo miaka 25 iliyopita Mzee Mengi alikuwa na wazo la kuwapa nafasi mashabiki kujumuika pamoja kuangalia burudani ya soka," alisema Gwaluma kutoka jijini Mwanza.

Alisema pia mashabiki wa soka walipata nafasi nyingine ya kushuhudia Fainali za Kombe la Dunia mwaka huo kupitia kituo chake cha televisheni cha ITV bila gharama yoyote.

### KLABU ZATUMA SALAMU

"Tarehe kama ya leo (jana) mwezi mmoja uliopita yaani Aprili 2 mwaka huu pale hoteli ya Serena muda wa saa 1: 00 tulikuwa na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Mzee wetu, Reginald Abraham Mengi, najiamkia asubuhi naambiwa mzee amefariki, inahuzunisha sana," alisema Haji Manara, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba.

Manara alisema kuwa anakumbuka marehemu Dk. Mengi alimweleza kutumia umaarufu aliokuwa nao kusaidia watu kiuchumi na kumtaka apambane kusaka fedha ili aweze kutumia vema umaarufu alionao.

"Tunajua kazi yako haina makosa, lakini turuhusu kwa unyenyekevu tumlilie baba na rafiki yetu mpendwa, wenyewe tulikuwa tukimwita Chairman. Pumzika kwa amani baba Mengi," alimaliza Manara.

Uongozi wa Pamba FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, ulisema katika taarifa yake kuwa umepokea kwa majonzi taarifa za kifo cha Dk. Mengi na ni pigo kwa wanamichezo wote hapa nchini.

"Katika kuthamini mchango wake kwenye michezo hasa mpira wa miguu, Klabu ya Pamba SC inaungana na Watanzania pamoja na familia ya Mzee Mengi katika msiba huu mkubwa uliowakuta," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Iliongeza kuwa Pamba inatoa pole kwa wadau wote wa michezo ndani na nje ya Tanzania ambao wameguswa na msiba huo uliotokea huko ughaibuni.

"Tunawapa pole wote walioguswa na msiba hu, tunamwombea subira katika kipindi hiki kigumu, poleni IPP, poleni familia ya Dk. Mengi," ilimaliza taarifa hiyo.

Klabu ya Lipuli FC ya Iringa maarufu "Wanapaluhengo" waliungana na wanamichezo wengine kuombeleza kifo cha Dk. Mengi ambaye alikuwa shabiki namba moja wa Serengeti Boys.

### MSULUHISHI YANGA

Katika kuonyesha kukerwa na hali ya makundi, marehemu Dk. Mengi wakati wa uhai wake aliamua kujikita katika mgogoro uliokuwapo katika klabu ya Yanga ambao ulipelekea kuzaliwa kwa makundi mawili.

Makundi hayo yalikuwa ni Yanga Kampuni ambayo ilikuwa inahamasisha klabu kubadilisha mfumo wa kiuendeshaji na wale waliokuwa wanapinga mabadiliko hayo ambao nao waliitwa Yanga Asili wakiwa chini ya kiongozi wao, marehemu, Yusuph Mzimba.

Jitihada za kumaliza mgogoro huo zilikuja kumalizika baada ya serikali kuzitaka klabu zote zifanye marekebisho katika katiba zake ili ziendane na hali halisi jambo ambalo leo hii watani zao, Simba wamefanikiwa.

### MWENYEKITI TAIFA STARS

Marehemu Dk. Mengi pia aliwahi kuongoza Kamati ya Ushindi ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) wakati ikisaka tiketi ya kucheza Fainali za Afrika za mwaka 1994.

Akiwa mwenyekiti wa kamati hiyo akishirikiana na mfadhili wa zamani wa Simba, Azim Dewji, Stars ilifanya vema kwa kushinda mechi zake zote za nyumbani.

Stars ilifanikiwa kuwafunga Algeria, Sudan na Uganda, lakini iliteleza kwenye michezo ya ugenini na kupoteza nafasi ya kushiriki fainali za mashindano hayo ambazo mwaka huu zitachezwa mwezi ujao Misri.

***Pumzika kwa amani mlezi wa Serengeti Boys.***

# Michezo


Ijumaa Mei 3, 2019

Nipashe




Madrid yajitosa kumwania Jovic

HABARI UK.30



# Wadau wa michezo wamlilia Dk. Mengi


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042